UKURASA WA 22

**RONALDO ATOLEWA KOMBE LA MFALME**




UKURASA WA 2

**TATHMINI KUFANYWA KUBORESHA MAFAO PSSSF, NSSF**

UKURASA WA 4

**MNH KUWEKA KAMBI MATIBABU WAGONJWA WENYE MAUMIVU MAKALI**



UKURASA WA 4

**DCEA KUKABILI DAWA ZA KULEVYA KWA KUTUMIA VIFAA VYA KISASA**

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Alhamisi Oktoba 31, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581846
www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Wabunge wakerwa mashirika mizigo

UKURASA 3



"Haiwezekani mpaka leo mashirika ya umma ya kibiashara misha-hara yao bado inatoka Hazina.

**Deogratius Mwanyika**



"Uteuzi wa wajumbe wa bodi za wakurugenzi wa mashirika na taasisi za umma uzingatie taaluma, ujuzi, weledi, uzoefu na tabia.

**Shamsi Vuai Nahodha**



"Mashirika ya umma ni lazima yajiendeshe kama ya binafsi ili yafanye vizuri.

**Joseph Tadayo**




Dereva wa kampuni ya mabasi ya Ahsante Rabi, Shedrack Swai (37), aliyesababisha ajali ili-yopoteza maisha ya watu tisa na majeruhi 54, eneo la Ukiriguru, Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, Oktoba 22 mwaka huu, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, akitolewa kituo kikuu cha polisi, jijini Mwanza jana, kwa ajili ya kupelekwa katika Mahakama ya Wilaya hiyo na kusomewa makosa 64, ikiwamo kuendesha gari kwa uzembe na kusababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa miundombinu na mali. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Dereva ajali iliyoua tisa akiri makosa 64 mahakamani

UKURASA 3

# Watoto waliookolewa ndoa za utotoni wafaulu darasa la saba

UKURASA 2




Scan hapa kutembelea chanel yetu

# Mafao PSSSF, NSSF kuboreshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kwa sasa inaendelea kufanya tathmini katika Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Mfuko wa Taifa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kuboresha mafao kwa kuzingatia uhimilivu wake.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu, Patrobas Katambi, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ngara (CCM), Ndaisaba Ruhoro.

Katika swali la msingi, alihoji serikali ina mkakati gani wa kuongeza kiwango cha pensheni kwa wastaafu nchini.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema ongezeko la kiwango cha pensheni kwa wastaafu hufanyika baada ya tathmini ya uhimilivu wa mifuko kama ilivyoainishwa kwenye masharti ya Kifungu cha 57 cha Sheria ya PSSSF na Kifungu cha 71B cha Sheria ya NSSF.

"Tathmini hii hufanyika kila baada ya miaka mitatu au kipindi chochote inapohitajika kufanyika kwa tathmini hiyo. Kwa sasa serikali inaendelea kufanya tathmini kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa sheria za mifuko," alisema.

Alisema serikali inawahakikishia wastaafu kuwa itaendelea kufanya tathmini kwa lengo la kuboresha mafao kwa kuzingatia uhimilivu wa mifuko na kwa mujibu wa sheria husika.

Katika swali la nyongeza, alisema kutokana na za maisha na kuna wastaafu wanaopokea pensheni chini ya Sh. 150,000 ambayo haitoshelezi kumudu gharama za maisha: "Ni kwanini kiwango cha kima cha chini cha mshahara wa serikali kilichowekwa kisiweke kima cha chini cha kutoa pensheni kwa wastaafu wanaopokea pensheni ndogo," alihoji.

Pia, alihoji serikali haioni kuna haja ya kufanyika tathmini hiyo kila baada ya mwaka mmoja badala ya miaka mitatu.

Akijibu maswali hayo, alisema utaratibu uliopo kwa hesabu za kitaalamu inaelekeza mifuko ya hifadhi ya jamii tathmini ifanyike kila baada ya miezi mitatu kwa sababu za kiuchumi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
MOSHI

SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA 82 YA 2023

MWANANANCHI ENGINEERING & CONTRACTING COMPANY (MECCO)................................MLETA MAOMBI

VERSUS

KILEMPU KINOKA LAIZER.............................MJIBU MAOMBI NA.1
STEPHEN KIMAN LAIZER.............................MJIBU MAOMBI NA.2
THOMAS SINYOCK LAITAYO .............................MJIBU MAOMBI NA.3
THOMAS SINYOCK LAITAYO .............................MJIBU MAOMBI NA.3.
THOMAS MORINGE MAKESEN.............................MJIBU MAOMBI NA.4
JULIUS KESOI LAITAYO.............................MJIBU MAOMBI NA.5
NOEL MAYASEK LAITAYO.............................MJIBU MAOMBI NA.6
RICHARD LERUNDA MOLLEL.............................MJIBU MAOMBI NA.7
NOAH KILEMPU LAIZER.............................MJIBU MAOMBI NA.8
SINJORE THOMAS LEITAYOK.............................MJIBU MAOMBI NA.9
AMIRI PANGANI.............................MJIBU MAOMBI NA.10
MONICA JACKSON.............................MJIBU MAOMBI NA.11
CHARLES KAAYA.............................MJIBU MAOMBI NA.12
LAZARO THOMAS .............................MJIBU MAOMBI NA.13
KUYA KIMANI.............................MJIBU MAOMBI NA.14
MAGUYA MELEJI.............................MJIBU MAOMBI NA.15
BARAKA KENYATTA.............................MJIBU MAOMBI NA.16

**KWA:**
**THOMAS SINYOCK LAITAYO ...................MJIBU MAOMBI NO.3**
**JULIUS KESOI LAITAYO...................MJIBU MAOMBI NA.5**
**NOEL MAYASEK LAITAYO...................MJIBU MAOMBI NA.6**
**NOAH KILEMPU LAIZER...................MJIBU MAOMBI NA.8**
**SINJORE THOMAS LEITAYOK ...................MJIBU MAOMBI NA.9**
**AMIRI PANGANI...................MJIBU MAOMBI NA.10**
**MONICA JACKSON...................MJIBU MAOMBI NA.11**
**CHARLES KAAYA...................MJIBU MAOMBI NA.12**
**LAZARO THOMAS ...................MJIBU MAOMBI NA.13**
**KUYA KIMANI...................MJIBU MAOMBI NA.14**
**MAGUYA MELEJI...................MJIBU MAOMBI NA.15**
**BARAKA KENYATTA ...................MJIBU MAOMBI NA.16**

**"POPOTE PALE MLIPO"**

Mnajulishwa kwamba shauri la maombi ya gharama tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa hapa Mahakama ya rufani Kanda ya Moshi tarehe 6/11/2024 saa tatu kamili asubuhi (06:00 mchana.)
Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa nyinyi wenyewe au mwakilishi wenu anayetambulika kisheria, maombi yatasikilizwa bila ya uwepo wenu.
Imetolewa na Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 23/10/2024.

J.J. KAMALA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI


# Watoto waliookolewa ndoa za utotoni wafaulu darasa la saba

**Na Elizabeth Zaya**

WATOTO wanne kati ya watano waliookolewa kuozeshwa mkoani Shinyanga, wamefaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, wakipata Daraja B na wawili Daraja C.

Mwenzao mmoja amepata Daraja E katika matokeo hayo yaliyotangazwa juzi na Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Watoto hao waliokolewa kwa nyakati tofauti wakiwa wamekatishwa masomo kisha kupelekwa katika kituo cha kusaidia watoto wanaokumbwa na madhila ya namna hiyo cha Agape kilichoko mkoani humo.

Baada ya kufikishwa katika kituo hicho, walirejeshwa shuleni kupitia Waraka wa Elimu Namba 2 wa Mwaka 2021 ulioruhusu wanafunzi wanaokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ujauzito, kurejea shuleni.

Utaratibu wa kurejesha wanafunzi hao waliokatisha masomo, ulianzishwa rasmi muda mfupi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani mwaka 2021 kwa kuagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutengeneza utaratibu maalumu wa kundi hilo kurejea shuleni.

Watoto hao walipelekwa katika Shule ya Msingi Mwapalala, Manispaa ya Shinyanga ili kuendelea kutimiza ndoto zao.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mlezi wa Kituo cha Agape, John Miyola, alisema amepata faraja kubwa baada ya kuona matokeo ya wasichana hao.

"Kwa kweli nimefarijika sana baada ya kuona matokeo ya wasichana hawa, ni watoto ambao walionekana kukata tamaa sana kutokana na yale waliyopitia, lakini tulipambana kuwarudisha katika mstari mzuri na kuwaambia wasikate tamaa, tunashukuru wanne wamefanya vizuri.

"Nilitamani wote wafaulu lakini haijawa riziki. Huyu mmoja hajafanya vizuri, amepata Daraja E ila hatujamkatia tamaa, tutafanya mpango arudie tena," alisema.

Miyola alisema kila mwaka anapokea zaidi ya wasichana zaidi ya 50 wanaokimbia kuozeshwa kutoka katika mkoa wa Shinyanga.

Mmoja wa mabinti waliofaulu, mwenye umri wa miaka 15 (jina linahifadhiwa) kutoka katika kijiji cha Rusanda, alisema alikatishwa masomo akiwa darasa la tano mwaka 2020. Alisema aliambiwa anahamishwa kutoka katika mkoa huo kwenda Kigoma kumfuata baba yake mzazi aliyekuwa akiishi huko.

Binti huyo alisema akiwa Shinyanga, alikuwa anaishi na mama yake mzazi ambaye alitengana na baba yake na baadhi ya mahitaji ikiwamo ya shule alikuwa akisaidiwa na mjomba yake.

Alisema baada ya kuambiwa anatakiwa amfuate baba yake, aliahidiwa kuchukuliwa uhamisho katika shule aliyokuwa akisoma awali na alikubaliana na uamuzi huo.

"Lakini cha kushangaza tulipofika Kigoma, mambo hayakuwa kama nilivyoahidiwa. Shule sikuendelea na nilipohoji, niliambiwa uhamisho wangu haukuchukuliwa. Lakini napo sikukaa sana, baba yangu akaniambia kwamba tunatakiwa kurudi tena Shinyanga kwa sababu Kigoma maisha ni magumu.

"Nilifurahi kwa sababu niliamini nikirudi nitaendelea na masomo yangu lakini haikuwa hivyo. Tumerudi ilikuwa mwaka 2021 mwanzoni, nikaomba kurudi kusoma lakini baba akasema haiwezekani kwa sababu tayari nimeshatafutiwa mchumba wa kunioa," alisema.

Anasema alikataa kwamba hataki kuolewa mpaka akaenda kwa mama yake kumweleza, lakini naye alimwambia kama tayari baba yake amefanya uamuzi huo, hana cha kumsaidia zaidi ya kukubali kwa sababu wako wenzake anaolingana nao wameolewa.

"Mwezi wa tano mwaka 2022 mchumba alikuja nyumbani, nikaitwa nikaenda na babu yangu, wakajitambulisha na wakaniuliza kama ninakubali kuolewa, nikanyamaza. Walivyoona sijajibu hata waliponiuliza mara mbili, mjomba aliniuliza kwa nini sitaki kuolewa napo sikumjibu chochote.

"Mama alimwambia mjomba, huyu hajatakaa tu kusema lakini amekubali, wakati mimi sitaki. Baadaye wakaondoka na mwezi wa sita wakatoa mahali lakini nikakaa mpaka mwezi wa nane ambao ndio ilikuwa harusi,: alisimulia.

Binti huyo alisema wakati sherehe ikiwa ukingoni watu wakitoa zawadi, askari walifika na kumkamata yeye na mama yake wakati huo baba na mjomba wake walipata upenyo na kukimbia lakini baadaye walikamatwa na kufikishwa kituo cha polisi.

Alisema baada ya mahojiano aliachiwa huru na kukabidhiwa kwa askari wa kike ambaye alimpeleka katika kituo cha Agape.

Binti mwingine mwenye umri wa miaka 16 (jina pia linahifadhiwa) ambaye amefaulu, alisema ametokea Kishapu pia mkoani Shinyanga, alikokuwa akiishi na mama yake, huku baba akiishi wilaya nyingine na mwanamke mwingine.

Alisema akiwa darasa la tatu, maisha yaliaanza kuwa magumu hadi kufikia kwenda kufanyishwa vibarua mashambani na fedha aliyopata ilisaidia mahitaji ya nyumbani kwa sababu mama yao alikuwa mgonjwa.

"Nikiwa darasa la nne, alijitokeza mwanamume kutaka kunioa ambaye alizungumza na mama na shangazi yangu. Nilikataa kuozeshwa kwa nguvu," alisema.

Alisema licha ya kumshirikisha shangazi ili kumsaidia, alimtaka akubali kwa kigezo kwamba upande wa mwanamume wana mali.

Kutokana na kukosa msaada, alisema alichukua uamuzi mgumu wa kukimbilia mjini ndipo alipowasiliana na dada ambaye aliwahi kufanya kazi kwake na alipomweleza yaliyomsibu, alimsaidia kwa kumkutanisha na mzee mmoja aliyemwunganisha na Agape.


**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES LTD**
**P.O.BOX 429 DODOMA-TANZANIA**
**OFFICE LOCATION: CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9**
**mabondojr@gmail.com 0715170553**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa mamlaka niliyopewa na Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA kituo cha DODOMA MJINI nitauza kwa mnada wa hadhara kiwanja na. 818, kitalu DA, Mtumba, kiwanja na. 876, Kitalu DA, Mtumba, na kiwanja na. 177, Kitalu J, Mtumba, Jiji la Dodoma ili kulipa fedha wanayodaiwa wadaiwa katika shauri la madai namba 144/2023 kati ya

**EDMUND ALFRED KAWEYA.................................MDAI**

**Dhidi ya**

1. **YUSTANCE WILSON KAWEYA ..................MDAIWA**
2. **ANDIPA WILSON KAWEYA........................MDAIWA**

Mnada utafanyika tarehe 08/11/2024 mahali viwanja vilipo, na muda ni kuanzia saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi (10:00) jioni kwa ratiba itakavyo tangazwa na gari la matangazo ya wazi

**Masharti ya mnada**
i. Mnunuzi atalipa 25% ya bei yam nada, na 75% atalipa ndani ya siku kumi na nne (14)asipofanya hivyo mnada utarudiwa tena, kiasi kilicholipwa hakitarudishwa
ii. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
iii. Atakayehitaji kuona viwanja kabla ya mnada, atapelekwa kwa gharama zake
iv. Dalali wa Mahakama ndiye mshusha nyundo ya mwisho

**KWA MAWASILIANO ZAIDI, PIGA SIMU 0715170553**

# Wabunge wakerwa mashirika mizigo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameeleza kukerwa na baadhi ya mashirika na taasisi za umma kujiendesha kwa ufanisi duni, kuendelea kutegemea ruzuku hali inayoisababishia serikali hasara.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23, inaonesha kuwa utegemezi wa mashirika ya umma umeongezeka kutoka Sh. bilioni 13.2 hadi 17.4.

Kutokana na hilo, serikali imeshauriwa kuangalia namna ya kuyafunga, kuyafilisi au kuyatafutia ubia na sekta binafsi.

Akichangia bungeni jana taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali (PAC) na ya Serikali za Mitaa ((PAC na LAAC) na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu uchambuzi wa ripoti hizo, Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika, alisema katika mashirika 35 ya kibiashara bado mashirika 17 yanapokea ruzuku ya serikali.

"Haya ndiyo mambo yaliyosababisha mageuzi na kwa nini baadhi ya mashirika kubinafsishwa? Kufanya biashara kuna taratibu zake na moja kubwa ni kurudisha mtaji na kufanya kazi kwa tija.

"Jambo hili tusilivumilie kwa muda mrefu. Haiwezekani mpaka leo hii mashirika ya umma ya kibiashara mishahara yao bado inatoka Hazina. Hili halikubaliki, si matumizi mazuri ya fedha za umma," alisema.

Mwanyika alisema serikali imeweka vigezo kwamba shirika au taasisi itoe kuanzia asilimia 15 ya mapato ghafi kama mchango lakini bado kuna baadhi yanashindwa.

"Hata yale yaliyotoa mwenendo unaonesha kumekuwa na kuteremka kwa gawio kwa mapato mashirika ambayo yamekuwa yanatoa gawio. Ukisoma ripoti hii mashirika kwa sasa yako zaidi ya 248 lakini najiuliza ni lini tumeunda mashirika yote hayo mengi?

Mwelekeo kwa sasa bado haujabadilika sana kwani bado kuna mashirika mengi yanaingiza hasara na hayajatambua uwekezaji wa serikali kwamba inatakiwa ipate faida kwa ajili ya Watanzania," alisema.

Alibainisha kuwa kuna mashirika ambayo yanatoa huduma yanavumiliwa lakini yako yanayofanya biashara yanatakiwa yashindane, yarudishe mtaji na kutoa gawio.

"Jambo lingine ambalo limejitokeza kuna kampuni za biashara zinaingiza hasara mpaka zaidi ya miaka mitatu mfululizo. Kwa utaratibu wa kibiashara, kampuni ikiingiza hasara kwa miaka mitatu mfululizo hiyo ni kampuni inayofilisika, isiendelee kuharibu rasilimali za nchi," alisema.

**WASTAAFU KUTEULIWA**

Mbunge huyo alisema kuna tatizo kubwa nchini la kutambua kazi na umuhimu wa bodi za wakurugenzi na kwamba bodi hiyo si sehemu ya kupeleka watu waliostaafu.

Naye Mbunge wa Kuteuliwa, Shamsi Vuai Nahodha, alipendekeza mambo sita yanayolenga kuondokana na matumizi mabaya ya fedha za umma na kutaja vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa kwenye uteuzi za wajumbe na watendaji wakuu wa mashirika na taasisi za umma.

"Uteuzi wa wajumbe wa bodi za wakurugenzi wa mashirika na taasisi za umma zizingatie taaluma, ujuzi, weledi, uzoefu na tabia. Watendaji wakuu wa mashirika ya umma wateuliwe kwa kuzingatia tabia zao, umahiri wao, uzoefu, elimu na mitazamo yao," alisema.

Alitaka serikali ipeleke watendaji wakuu kwenye mafunzo ya kikazi nje ya nchi hasa kwenye mashirika makubwa ya kihasibu ili wajifunze namna ya kuendesha mashirika hayo.

Pia aliomba serikali kuimarisha mifumo yake kwenye kutathmini utendaji wa mashirika na iongeze kasi ya kutekeleza agizo la kuimarisha matumizi ya mifumo ya serikali isomane ili kudhibiti udanganyifu.

Mbunge wa Mwanga (CCM), Joseph Tadayo, alisema mashirika ya umma ni lazima yajiendeshe kama ya binafsi ili yafanye vizuri.

"Kwa bahati mbaya bodi zetu nyingi ni zile ambazo hazina umahiri na sekta wanazozisimamia, hawawezi kutupa matokeo tunayoyataka na kumekuwa na malalamiko ya hapa na pale kwamba serikali inawaingilia.

"Lakini bodi ambayo ina uwezo haiwezi kukubali kuingiliwa na serikali. Ni bora wajiuzulu kama wanaona serikali inawaingilia," alisema.

Tadayo alisema bodi lazima zitambue kazi zao ni kuongoza ili kuleta faida na zisimamie mashirika yafanye miradi inayoleta faida.

## Tanzania kuwa na kituo cha ubunifu

**Na Mwandishi Wetu,** VALLETTA-MALTA

TANZANIA inaanzisha kituo cha kitaifa cha ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), ili kujenga uwezo na kuchochea ubunifu wa kidijitali nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, aliyasema hayo jana wakati akizungumza kuhusu mkutano wa Bodi ya Wadau wa Usimamizi wa Ubunifu ya Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (ITU) wakati wa Kongamano la Ubunifu kati ya Oktoba 28 na 30, mwaka huu.

Alisema kituo hicho kinalenga kuchochea mabadiliko ya ikolojia nzima ya ubunifu Tanzania.

Aidha, aliongeza kuwa kituo hicho ni sehemu ya mtandao wa vituo vya ubunifu vinavyoanzishwa na Shirika la mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU), katika ngazi za dunia nzima, kanda na kitaifa.

Dk. Bakari ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya ITU, alisema kituo hicho kitatoa msaada wa kiufundi kwa vituo vya ubunifu. Akiwasiliana kutoka Valetta, Malta kulikofanyika mkutano huo, alisema kituo hicho kinasimamiwa na Tume ya TEHAMA Tanzania.

"ITU ilianzisha Ushirikiano wa Ubunifu na Ujasirimali Januari, 2023 ili kuweka mfumo wa kupunguza mapengo ya ubunifu kwenye nchi wanachama

"Tanzania, kupitia TCRA, inatekeleza mpango wa kuendeleza ubunifu na uvumbuzi kwa kutoa raslimali za mawasiliano bure kwa wajasiriamali na kampuni changa kujaribu miradi yao," alisema.




Wajumbe wa Bodi ya Wadau wa Usimamizi wa Bunifu ya ITU, wakiwa pamoja wakati wa Kongamano la Ubunifu, lililofanyika katika mji wa Valletta, Malta, juzi. Tanzania iliwakilishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabir Bakari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dereva ajali iliyoua tisa akiri makosa 64 kortini

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

DEREVA wa Kampuni ya Mabasi ya Ahsante Rabi, Shedrack Swai (37), anayedaiwa kusababisha ajali iliyoua watu tisa na kujeruhi 54, amekiri makosa 64 katika Mahakama ya Wilaya ya Misungwi.

Dereva huyo alipandishwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Esther Marick, na kusomewa shtaka katika kesi ya trafiki namba 30855/2024 inayomkabili.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Ramson Salehe, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Lilian Meli, alidai mahakamani hapo kuwa mshtakiwa alitenda makosa hayo kinyume cha Kifungu cha 41, 63 (2) (b) na 27 (1) cha Sheria ya Usalama Barabarani Namba 168, Marejeo ya Mwaka 2002.

Alidai kuwa Swai alisababisha ajali hiyo Oktoba 22, mwaka huu, eneo la Ukiliguru, Misungwi, mkoani Mwanza.

Mwendesha mashtaka alidai dereva huyo anakabiliwa na shtaka la kuendesha gari kwa uzembe katika barabara ya umma lenye makosa 64 yakiwamo kuendesha gari kwa uzembe, kusababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa miundombinu na mali.

Alidai kuwa siku ya tukio, mshtakiwa akiwa dereva wa basi lenye namba za usajili T 458 DYD aina ya Yutong, aliendesha kwa uzembe katika barabara ya umma ya Mwanza - Shinyanga katika kijiji cha Ukiriguru.

Alidai kuwa alilipita gari lingine bila kuchukua tahadhari na matokeo yake kuligonga basi lenye namba za usajili T 281 EFG aina ya Yutong na kusababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali.

Baada ya kumsomea shtaka hilo, mshtakiwa alikiri kutenda makosa hayo yote 64 ndipo Wakili wa Serikali Mwandamizi Meli aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

Hakimu Marick alimweleza mshtakiwa kuwa shtaka linalomkabili linadhaminika, hivyo kumtaka kuwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka serikali ya mtaa, kitambulisho cha taifa (NIDA) na bondi ya maneno ya Sh. milioni tano kila mmoja.

Mshtakiwa alishindwa kukidhi masharti ya dhamana baada ya mdhamini mmoja kukosa kitambulisho halisi cha NIDA, hivyo kupelekwa rumande katika Gereza la Butimba, Mwanza hadi masharti hayo yatakapotimizwa.

Hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 5, mwaka huu, itakapoitwa kwa ajili ya kusomewa hoja za awali.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi ya Wizara ya Ujenzi yenye makao yake makuu Morogoro. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa Vikundi vya Wanawake na Vijana(Makundi maalumu) katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)** 25/11/2024 – 21/12/2024 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**
Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:

Kozi hii, Washiriki watajifunza maada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kumwezesha Wanawake na Vijana (washiriki) kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hii yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:
i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**
a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**
Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi kwa gharama ya ada kiasi cha Tsh. 700,000.

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi tajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

S.L.P 963, MOROGORO.
Simu : 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957, MBEYA.
Simu : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404/0765251509
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com


# MNH kufanya kambi ya matibabu wagonjwa wenye maumivu makali

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) Upanga kwa kushirikiana na Taasisi ya ROAD2IR ya Marekani, itafanya kambi maalumu ya kwanza nchini ya matibabu ya wagonjwa wenye maumivu makali ya viungo kupitia njia ya kisasa ya tiba mionzi.

Kambi hiyo ya uchunguzi na matibabu itafanyika kwa wagonjwa pia wenye maumivu makali sehemu mbalimbali za mwili kwa njia hiyo ya kisasa itakayoongozwa na Daktari Bingwa Mbobezi wa matibabu hayo duniani, Prof. David Prologo kutoka Hospitali ya Emory Health Care ya Marekani.

Tiba radiolojia ni aina ya taaluma ya matibabu ambayo daktari bingwa mbobezi hutumia teknolojia ya picha za uchunguzi za (Angio-Suite, CT, Xray, Ultrasound) kumwongoza kufanya uchunguzi au tiba kupitia matundu madogo mwilini bila kufanya upasuaji.

Akizungumzia jana kuhusu kambi hiyo, Bingwa Mbobezi wa Tiba Radiolojia MNH, Dk. Erick Mbuguje, alisema itahusisha matibabu ya wagonjwa wenye maumivu makali ya aina zote yaliyogawanyika katika makundi makuu mawili; maumivu ya mgongo na maumivu ya sehemu nyingine za mwili.

"Katika kundi la kwanza ni wagonjwa wenye maumivu makali ya mgongo yasiyosababishwa na saratani ni pamoja na pingili zilizosagika, kuvunjika au kupukutika. Matibabu ya maumivu hayo yahusishi upasuaji, diski zinazokandamiza mishipa ya fahamu.

"Hivyo maumivu kusambaa sehemu za miguuni ambayo hayatibiki kwa upasuaji na wagonjwa wenye maumivu yatokanayo na maungio ya pingili na kuongeza kuwa kwa wagonjwa wenye maumivu ya mgongo yatokanayo na saratani iliyosababisha kuvunjika kwa pingili au kubana kwa mishipa ya fahamu nao watahudumiwa," alisema.

Dk. Mbuguje alisema kundi la pili ni wagonjwa wenye maumivu makali ya viungo vingine vya mwili ambayo hayajasababishwa na saratani kwenye magoti, mabega, nyonga.

Alisema maumivu hayo ni ambayo matibabu ya maumivu hayo hayaondolewi kwa njia ya upasuaji, hivyo katika kundi hilo wenye maumivu mengine yatokanayo na saratani mbalimbali mfano kongosho nao pia, watanufaika na huduma hiyo.

"Huduma za uchunguzi na matibabu zitafanyika kuanzia Novemba 4 hadi 15 Novemba, mwaka huu, Idara ya Radiolojia iliyoko karibu na jengo la Utawala, chumba namba 24, kuanzia saa mbili asubuhi hadi 11 jioni.

"Huduma zitatolewa kwa utaratibu wa kawaida wa hospitali. Wagonjwa wote wenye changamoto hizo wanaombwa kuwasiliana moja kwa moja na Dk. Erick Mbuguje 0764497642, Dk. Azza Naif 0713264350 na Dk. Mwivano Shemwetta 0755217298 ili kupata taarifa zaidi," alisema.

# DCEA kukabili dawa za kulevya kwa kutumia vifaa vya kisasa

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema kuwa inahitaji kuwa na vifaa vya kisasa wanavyoweza kutembea navyo wakati wa kufanya ukaguzi ili viwawezeshe kupima na kubaini dawa hizo kwa uharaka ikiwamo aina mpya ambazo zimeanza kutumika.

Kamishna kutoka mamlaka hiyo, Peter Patric, aliliambia gazeti hili wakati wa maadhimisho ya 'Forensic day' kuwa ripoti ya hali ya dawa za kulevya ya mwaka 2023 ilionesha kumekuwa na aina mpya ya dawa hizo 1,184 zilizoingia kwenye soko la dunia.

Kutokana na hali hiyo, alisema wanahitaji vifaa hivyo kupima watu waliotumia ili kuhakikisha ni dawa gani aliyotumia, akieleza kuwa itawasaidia kujua aina yoyote ya dawa za kulevya zinazoingia na kutumika nchini.

"Tunaweza kufanya utafiti tukaenda mahali hata kwenye 'bar' tukatoboa sehemu walevi wanapokojoa na kuchukua sampuli ya kila mkojo, hapo tunaweza kugundua kuna dawa nyingi zimeingia nchini, ambazo hatujawahi kuzikamata, lakini sio kwamba hatujakamata kwasababu sisi ni wazembe hapana! Ni kwasababu hazitambuliki.

"Pia dawa hizo huwezi kuzitilia mashaka kwasababu haziko kwenye jedwali la dawa zinazodhibitiwa, kwahiyo matokeo yake zinasababisha madhara makubwa kuliko zile ambazo tulizizoea, sasa hivi tunasikia kunatokea vifo vingi sana kwa waraibu wa dawa za kulevya kwasababu ya kuzidisha kiwango," alisema Patrick.

Aidha, alisema mamlaka hiyo ina mikakati mikuu minne, ikiwamo kupunguza uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini, kupunguza mahitaji kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yake ili watu wasijiingize kwenye matumizi ya dawa hizo.

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**

*benki kwa maendeleo yako*

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Robo Mwaka Mwaka iliyopita 30-Jun-24 |
|---|---|---|---|
| **A. MALI** | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 13,960 | 15,868 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,831 | 12,843 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 38,419 | 38,015 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,645 | 2,775 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 26 | 19 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 108,678 | 118,473 |
| 12 | Mali Nyingine | 16,327 | 13,975 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 13,339 | 13,843 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **208,264** | **215,851** |
| **B. DHIMA** | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 25,064 | 28,780 |
| 18 | Amana za Wateja | 119,780 | 124,902 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 2,221 | 812 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 0 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 5,400 | 4,544 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 37 | 525 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,496 | 2,175 |
| 27 | Dhima Nyingine | 14,822 | 15,168 |
| 28 | Madeni | 20,070 | 17,250 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **189,892** | **194,156** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **18,372** | **21,695** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 27,797 | 27,797 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (18,188) | (18,881) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (5,292) | (3,799) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 14,055 | 16,577 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,372** | **21,695** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 5,204 | 1,153 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 9,037 | 9,707 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,783 | 4,474 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 243 | 243 |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8.8% | 10.1% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.9% | 7.9% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76.4% | 77.6% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.2% | 56.8% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 71.9% | 73.8% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -4.8% | 2.6% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -3.5% | 2.3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-24 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **Mapato ya Riba** | **7,490** | **7,377** | **21,984** | **21,017** |
| 2 | Gharama za Riba | (2,710) | (2,052) | (7,204) | (6,099) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **4,780** | **5,326** | **14,780** | **14,918** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,156) | (505) | (3,347) | (691) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,362** | **1,824** | **5,242** | **6,183** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 148 | 121 | 721 | 418 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 864 | 1,148 | 3,233 | 3,296 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 350 | 555 | 1,287 | 2,468 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,479)** | **(7,148)** | **(21,967)** | **(20,725)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (3,098) | (3,744) | (11,043) | (11,054) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (3,380) | (3,404) | (10,924) | (9,671) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,493)** | **(503)** | **(5,292)** | **(316)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | 56 | - | (0) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,493)** | **(447)** | **(5,292)** | **(316)** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,493)** | **(447)** | **(5,292)** | **(316)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 253 | 368 | 253 | 368 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (54) | (16) | (190) | (11) |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | **17** | **18** | **17** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.8% | -1% | -3.3% | -0% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -29.8% | -7% | -35.2% | -2% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 105.5% | 100% | 109.7% | 98% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12.4% | 15% | 12.8% | 14% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/ MWAKA ULIOISHIA 30.09.2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-24 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-24 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,493) | (3,168) | (5,292) | (316) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 637 | 626 | 1,880 | 1,600 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 7,966 | (6,242) | (3,855) | (6,694) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | (24) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (7,428) | 3,954 | (3,568) | 17,107 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (500) | - | (450) | 3,133 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 344 | 1,469 | 1,637 | (4,042) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,209) | (1,156) | (2,544) | (2,263) |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | (19) |
| | - Mengineyo (bainisha) | (1,398) | 632 | (775) | 1,481 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | (3,081) | (3,885) | (12,966) | 9,964 |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (133) | (268) | (858) | (2,933) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | 3 | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | 96 | (143) | (393) | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | (37) | (412) | (1,249) | (2,933) |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | 5,663 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 2,820 | 2,606 | 11,720 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (2,208) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | 2,820 | 2,606 | 11,720 | 3,455 |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (298) | (1,690) | (2,495) | 10,486 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 24,745 | 26,435 | 26,942 | 19,266 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/ Mwaka** | 24,447 | 24,745 | 24,447 | 29,753 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Hisa za Upendeleo | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2024 | 27,797 | 11,623 | 2,432 | (19,215) | 2,856 | - | 25,493 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | (5,292) | - | - | (5,292) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | 2,856 | (2,856) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | (1,829) | - | - | (1,829) |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2024** | 27,797 | 11,623 | 2,432 | (23,480) | - | - | 18,372 |
| Mwaka Uliopita | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2023 | 27,797 | 5,960 | 2,432 | (15,276) | 930 | - | 21,844 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | - | (316) | - | - | (316) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | 5,663 | - | - | - | - | 5,663 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | (1,557) | 1,557 | - | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2023 | 27,797 | 11,623 | 2,432 | (17,148) | 2,487 | - | 27,191 |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2024**

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita


| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Silvest Arumasi **(Mkurugenzi Mtendaji)** | ____________ | ____________ |
| Mr. Peter Urassa **(Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha)** | ____________ | ____________ |
| Mr. Samwel Kimosso **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | ____________ | ____________ |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Ms.Catherine Nchanasaa Kimaryo | ____________ | ____________ |
| 2. Prof. Josephat Daniel Lotto | ____________ | ____________ |

+255 (746) 811 510

support@acbbank.co.tz | www.acbbank.co.tz



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upungufu wa maji Dar, Pwani upatiwe ufumbuzi wa kudumu

**MAENEO** mbalimbali ya mikoa ya Dar es Salaam na Pwani hasa yale yanayopata maji kutoka mtambo wa Ruvu Juu, kwa muda sasa yamekumbwa ya upungufu wa huduma hiyo. Si jambo la ajabu katika baadhi ya maeneo hayo kusikia vilio vya kukosa maji kwa wiki moja au zaidi.

Sababu kubwa iliyotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) takriban wiki mbili zilizopita ni kupungua kwa uzalishaji kutokana na upungufu wa maji katika Mto Ruvu ambao ndio tegemeo kubwa kwa upatikanaji wa huduma hiyo. Kwa ujumla, taizo kama hilo hujitokeza zaidi majira ya kiangazi kutokana na kupungua kwa kina cha maji kwa kuwa mvua inakuwa imekatika, hivyo kusababisha baadhi ya mito inayoulisha Mtu Ruvu kuwa na kiasi kidogo cha maji.

Licha ya tatizo hilo, kupungua kwa maji kwenye mto huo, kunatokana na shughuli za kibinadamu kama kilimo na ufugaji zinazofanyika kwenye vyanzo vya maji pamoja na uchafuzi wa mazingira. Wakati wa uongozi wa Hayati Rais John Magufuli, tatizo hilo liliwahi kujitokeza na wananchi kuwa katika adha kubwa ya kupata huduma hiyo na serikali iliingilia kati na kupiga marufuku shughuli za kibinadamu na hatimaye wananchi wakaondokana na tatizo hilo. Pia katika serikali ya sasa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ilitolewa amri ya kuondolewa kwa watu wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye Mto Ruvu na maji yakarejea kama kawaida.

Mbali na makatazo yaliyotolewa na viongozi wakuu wa nchi kuhusu tatizo hilo, DAWASA pia ilisafisha baadhi ya visima katikati ya Dar es Salaam vilivyokuwa havifanyi kazi na kupunguza adha waliyokuwa nayo wananchi.

Wakati hali ya sasa ikiendelea na Wizara ya Maji kupitia Waziri wake, Juma Aweso, kuwapa wananchi matumaini kama alivyosema hivi karibuni kwamba mambo yatakuwa maziri muda si mrefu, ni muda mwafaka sasa wa DAWASA kuwa na mipango endelevu ya kuhakikisha huduma ya maji inakuwa endelevu. Kwa maneno mengine, DAWASA inapaswa kuwa na mipango ya muda mrefu ya kuwezesha upatikanaji wa maji.

Miongoni mwa mipango hiyo ni kuangalia uwezekano wa kuwa na vyanzo vipya vya maji badala ya kutegemea vile vilivyopo pekee. Pia kumekuwa na taarifa kwamba mtambo wa Ruvu Juu unaotumika kuzalisha bidhaa hiyo ni wa muda mrefu, hivyo hauna ufanisi wa kutosha. Kama ni kweli DAWASA ina mpango gani wa kuhakikisha inakuwa na mtambo mpya na wa kisasa ambao utazalisha maji kwa wingi?

Aidha, kama inavyoeleweka kuwa maji ni bidhaa adimu kwa matumizi ya kila siku kwa binadamu na mamlaka hiyo inatoa huduma yenye mtazamo wa kibiashara, ni vyema ikawa na maono ya kuwa na huduma endelevu kwa kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi.

Watendaji wa DAWASA wanapaswa kubadilika kifikra kwa kufanya kazi kisasa zaidi badala ya mazoea ya miaka nenda miaka rudi. Kama maji hupungua wakati wa kiangazi, kama ilivyo sasa, na wananchi kupata shida, watendaji wa mamlaka hiyo wachukue hatua ya kuwa na visima pia ambavyo vitasaidia kupunguza tatizo kwa wananchi.

Haiwezekani tatizo likawa linajirudia na watendaji wakawa wanajua sababu na kutoa majibu yale yale kila mwaka badala ya kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu upatikanaji wa maji. Kama ambavyo imekuwa ikielezwa kuwa sababu ni kupungua kwa maji katika Mto Ruvu ambao wakati wa masika hufurika, kwa nini kipindi hicho mamlaka isivune maji ya kuyahifadhi kwa ajili ya matumizi ya baadaye?

Ni vyema hatua madhubuti zikachukuliwa kupunguza au kumaliza tatizo la maji katika mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani ambayo yanahudumiwa na DAWASA.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Pilly Kigome

## Muungwana Lazima Nilonge

# Naungana na kilio chao wadau, wenye dhamana kuwashika mikono vijana

**KUNA** kundi la vijana katika jamii, ambalo ni muhimu katika ujenzi wa taifa, kwa kuwa lina nafasi ya kutegemewa, kwani ni nguvukazi sahihi katika ustawi wa taifa.

Kundi hilo ni pana, linategemewa na katika kila nyanja, likitazamwa kuanzia ngazi ya familia, serikali, mashirika, taasisi zikiwamo asasi za kiraia katika kulijengea uwezo. Hiyo ni kwa kuwa ndio nguvu kazi inayoleta tija kuliko makundi yote, mtazamo hapo linatakiwa kuwa kundi linaloangaliwa zaidi, kwani ndio ustawi wa jamii kwa ujumla.

Asasi za kiraia kwa jina lake maarufu azaki za kiraia, jumla yake 300 wakati zimeumiza vichwa kwa pamoja na kwa kulitakafari kundi hilo na kuliwekea mikakati.

Hapo kuna mapendekezo kadhaa ajenda yao ya Uchaguzi wa Serikali ya Mitaa Mwaka 2024 hadi 2029, waliyoikabidhi Oktoba mwaka huu kwa vyama vya siasa.

Ndani yake wamelitazama kwa kina kundi hilo, ili kuhakikisha ilani hiyo inalipigania kundi hilo lipate kuangaliwa zaidi, kutokana na umuhimu wake.

Azaki za kiraia zinazotetea haki za binadamu zilitoa tamko kuhusu kundi hilo la vijana wakitaka kuwapo uanzishwaji wa fursa za ajira na kuiwekea mifumo rafiki ya mchakato wa uombaji na upatikanaji ajira hizo, ndani ya sekta za umma na binafsi.

Hapa tujiulize, je kwa kundi hili kuna mifumo rafiki iliyowekwa katika uombaji na upatikanaji wa ajira katika sekta hizo kwa vijana wa mijini na vijijini?

Kama Magali hapo kuna ukweli, tupige hatua nyingine ya kuhoji namna mifumo hiyo iko rafiki kwa kundi hilo. Naipa kongole serikali, kutokana na uanzishwaji huo unaowawezesha vijana wapate ajira.

Lakini hapo hapo, kama mazingira hayo hayapo, basi kwa juhudi hizi naamini mifumo hiyo ya fursa za ajira iwe na usawa kati ya vijana wa mijini na vijijini na iwe na usawa kati ya waliokuwa nacho na wasiokuwa nacho, ili fursa hizo ziwafikie vijana wote.

> **Vilevile tumeona azaki hizo kwa pamoja, zinaitaka serikali itekeleze programu za uwezeshaji vijana usio na ubaguzi kwa misingi ya kiitikadi.**

Tunaona pia azaki hizo zimetaka kuboreshwa kwa mfumo wa elimu kwa vijana, wanapataje elimu na mafunzo kwa vitendo yanayowapa ujuzi na maarifa ya kuwawezesha kuwa wabunifu na zaidi kuwawezesha kujiajiri.

Kwa upande wangu, pendekezo hilo liko sawa na kwani elimu ikiboreshwa vyema kwa upande wa vijana itakuwa 'bomba', itapendeza! Kwani nadharia 'vijana ni taifa la leo' imegeuka, si 'la kesho' tena kutokana na zama tulizoko.

Aidha ilani ya wadau wanaharataki imedai kuanzishwe utaratibu wa kuwapa nafasi vijana kushiriki kwenye michezo inayokuza na kuendeleza vipaji vyao, kuanzia ngazi za shule hadi vyuoni, waraisishe vipaji vyao na taaluma.

Vilevile tumeona azaki hizo kwa pamoja, zinaitaka serikali itekeleze programu za uwezeshaji vijana usio na ubaguzi kwa misingi ya kiitikadi. Hapo ni kuwapa fursa wote kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kujipatia kipato.

Pia, napo naunga mkono hoja kama juhudi hizi walizopendekeza asasi hizo, basi tutakuwa na taifa lenye tija, kwa kuwa programu hizo zikianzishwa vijana ambao ndio taifa la kesho wataweza kujitengenezea vipato visivyo na mwisho.

Walitaka uandaliwe mfumo wa kuwezesha vijana wote kushirikiana katika shughuli za uchumi na kupata ujira stahiki bila kunyongwa.

Viongozi waanzishe utaratibu wa kuwatambua vijana wenye vipaji na ubunifu katika maeneo tofauti na kuviendeleza waweze kuongeza thamani ya vipaji hivyo viwaingizie kipato.

Ilani imelitazama hilo kwa kina kundi hili la vijana na kulitetea vyema, ili kulitaka liwe na ustawi kwa kuwa ndio taifa la leo na la kesho naunga mkono hoja.

Ilipendekezwa na kutengenezwa na zaidi ya asasi za kiraia 300 na iliwakilishwa ndani vya vyama vya siasa na Mratibu Kitaifa wa Mtandao wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) Onesmo Olengurumwa.

# JKCI: 80% wagonjwa moyo huwa hatarini

**Na Zanura Mollel**

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Tulizo Shemu, ametoa wito kwa Watanzania kujitokeza kupima afya ili kubaini tatizo na kuwahi matibabu.

Alisema upimaji ni bure ambao ulianza juzi na kumalizika jana katika tawi la Kawe, jengo la Mkapa Health Plaza, lengo ni kuchukua hatua haraka kudhibiti magonjwa yakiwamo ya moyo.

"Dunia nzima imeweza kudhibiti magonjwa mbalimbali, lakini gonjwa hili la moyo limeonekana kusababisha vifo vya watu wengi kwa kukosa matibabu na wakati mwingine gharama kuwa kubwa," alisema Dk. Shemu.

Pia, upimaji wa afya ya moyo utasaidia watu kubaini hali zao na kuchukua hatua mapema ili kuepuka tatizo kuwa kubwa baadaye.

Dk. Shemu alisema upo uhusiano mkubwa kati ya shinikizo la juu la damu na ugonjwa wa moyo, pale shinikizo linapokuwa juu hupelekea moyo kufeli kusukuma damu, asilimia 80 ya wagonjwa wa ugonjwa huo hawafiki miaka mitano hufariki.

"Shinikizo la damu la kawaida ni 120/80 unapokuwa 140/100 hili ni shinikizo la juu, mgonjwa anatembea hatua moja anahema sana anakuchoka sababu ya tatizo hilo, hata hivyo, msongo wa mawazo ni moja ya sababu ya tatizo la ugonjwa wa moyo," alisema Dk. Shemu.

Dk. Shemu alisema takwimu za Wizara ya Afya kupitia MTUHA (DHIS-2) zinaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko la asilimia 9.4 kwa wagonjwa wa moyo na shinikizo la damu pekee kutoka wagonjwa milioni 2.5 mwaka 2017 hadi wagonjwa milioni 3.4 mwaka 2022.

Alifafanua kuwa kwa wagonjwa wanaotibiwa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ambayo inatoa tiba bobezi ya magonjwa ya moyo kati ya wagonjwa 125,927 waliotibiwa mwaka 2023, asilimia 42 sawa na wagonjwa (52,900) walikuwa na shinikizo la juu la damu.

"Hapa nchini watu wengi wanasumbuliwa na ugonjwa wa shinikizo la damu, lakini hawatambui kuwa na ugonjwa huu kwani hawajapima, asilimia 30 ndio waliopima na kujitambua kuwa na ugonjwa huu, asilimia tisa wanajijua kuwa na ugonjwa huu na kuendelea na matibabu kati ya hawa asilimia nne wameweza kudhibiti msukumo wao wa damu mwilini," alisema Dk. Shemu.

Mwenyekiti wa jukwaa la wahariri, Deodatus Balile, aliwaasa waandishi wa habari na wahariri kufanyakazi zao kwa weledi ili kuepukana na msongo wa mawazo ambao unatajwa kuwa miongoni mwa chanzo cha tatizo la ugonjwa wa moyo.

Alisema wakati mwingine mhariri uchapisha habari inayofurahisha upande mmoja na kuumiza upande mwingine, hujikuta akipitia misukosuko ya kikazi hali inayosababisha msongo wa mawazo na matatizo ya kiafya kwa mhariri.

Alisema, si kila habari inaulazima wa kuchapishwa ili kulinda afya ni vyema kuachana na habari zenye kuleta msongo wa mawazo.

Balile anasema mataifa ya nje yamekua yakitoa mafunzo kwa waandishi na wahariri kuandika habari ambazo zikifuatiliwa nchini mwao hawaziripoti na zimeonekana kuwaingiza waandishi na wahariri katika matatizo makubwa.

## Mikakati kutokomeza polio yaanikwa

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA imeweka mikakati madhubuti ya kuzuia na kutokomeza ugonjwa wa polio, ikiwa ni hatua ya kumaliza wagonjwa wapya nchini.

Mikakati hiyo imewekwa na nchi ikiwa ni njia ya kukabiliana na ugonjwa huo ambao hivi karibuni, umeripotiwa katika nchi za Kenya, Uganda, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Vida Makundi, aliyasema hayo juzi katika Mkutano wa 34 wa siku nne wa Ukanda wa Afrika wa Kutokomeza Ugonjwa wa Polio, jijini Dar es Salaam.

Alisema Tanzania mgonjwa wa mwisho kuripotiwa ilikuwa mwaka 1996 na kuanzia hapo hakuna aliyebainika. Ili kuudhibiti wanatoa chanjo kwa watoto wote na wanafanya ufuatiliaji wa karibu kubaini endapo kuna dalili za ugonjwa huo kwa watoto chini ya miaka 15, na kukusanya sampuli katika mipaka ya nchi ili kugundua maambukizi mapya.

"Katika kikao hiki, tutawaelezea wenzetu mikakati tuliyoweka na wao wajifunze na sisi tutajifunza kutoka kwao, tunaweka nguvu za pamoja kuhakikisha dunia haina polio 2030," alisema Dk. Makundi.

Mratibu wa Kutokomeza Polio Kanda ya Afrika, Jamal Ahmed, alieleza kuwa mkutano huo una lengo la kujadili mbinu za kupambana na virusi vinavyosambaa kwa kuvuka mipaka, na kuanzisha mikakati ya kukomesha ugonjwa huo ifikapo Desemba 2025.

Ahmed alisema lengo lao ni kuhakikisha watoto wote katika ukanda wa Afrika wanakuwa salama na wataweka hatua za dharura za pamoja kuutokomeza ugonjwa huo.

Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Hafidhi, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mkutano huo alisisitiza kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa kuondoa polio na kwamba ili nchi iwe salama zaidi, ni muhimu majirani pia kuongeza juhudi kupambana na ugonjwa huo.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi ambao orodha yao ipo hapa chini waliolipia viwanja kwa nyakati tofauti eneo la Kikombo Kitalu "DA" na "N" kupitia benki, ila taarifa zao zinamapungufu ya majina, namba ya kiwanja na kitalu wafike ya Halmashauri iliyopo Manispaa ya zamani sehemu ya **mauzo ya viwanja** kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao.

Muda wa utekelezaji ni kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2024 hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

Kushindwa kufanya hivyo, umiliki huo hautatambulika tena.

**ORODHA YA MAJINA YENYE TAARIFA PUNGUFU**

| NA | JINA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher Kasung | 10,000.00 |
| 2. | Mbaga Iyombe | 1,000,000.00 |
| 3. | Veisi Maineko | 42,000.00 |
| 4. | George Abel Ngab | 300,000.00 |
| 5. | Ngalawe Hassan Ramadha | 6,931,641.00 |
| 6. | Esther Mpangala | 5,000,000.00 |
| 7. | Victoria Mgala | 400,000.00 |
| 8. | Godfrey K. Msongwe | 9,096,340.00 |
| 9. | Eliaza Mangera Wangwe | 5,148,000.00 |
| 10. | Florence N. Kebwe | 2,515,000.00 |
| 11. | Ali Hussein Habib | 338,300.00 |
| 12. | Joseph Lukumbika | 265,000.00 |
| 13. | Rosina J Delima | 2,249,554.00 |
| 14. | Kelvin Mlambalamba | 1,200,000.00 |
| 15. | Starphod Marwa | 1,000,000.00 |
| 16. | Ally H. Thabit | 3,000,000.00 |
| 17. | Mariam Tawakel | 10,000.00 |
| 18. | Jeremia Baha | 255,000.00 |
| 19. | Shani Mwaruka | 400,000.00 |
| 20. | Ramadhan N Simba | 50,000.00 |
| 21. | Ally Habiba Thabit | 3,000,000.00 |
| 22. | Job Ndalo | 100,000.00 |
| 23. | Giligoli A Ndaro | 100,000.00 |
| 24. | Gloria Reuben Ndaro | 80,000.00 |
| 25. | Magreth W Luma | 10,000.00 |
| 26. | Chedi Ng'enda | 21,729,382.00 |
| 27. | Sospeter N Marco | 2,500,000.00 |
| 28. | Geophrey Mtweve | 1,150,000.00 |
| 29. | Leonary Kimario | 24,000.00 |
| 30. | Lilian Sebastian | 1,625,000.00 |
| 31. | Anna Elisamehe | 400,000.00 |
| 32. | Olais Peter | 300,000.00 |
| 33. | Mussa Deogratius Limb | 4,566,560.00 |
| 34. | Marium | 225,000.00 |
| 35. | Rainer | 4,607,934.00 |
| 36. | George | 100,000.00 |
| 37. | Jafari | 500,000.00 |
| 38. | Dann | 10,000.00 |
| 39. | Victoria | 1,015,000.00 |
| 40. | Jona | 50,000.00 |
| 41. | Alvin | 677,100.00 |
| 423. | Christina | 700,000.00 |
| 43. | Tina | 100,000.00 |
| 44. | Doreen | 300,000.00 |
| 45. | Kelvin | 1,500,000.00 |
| 46. | Innocent | 1,000,000.00 |
| 47. | Mabrouk | 100,000.00 |
| 48. | SHM | 1,000,000.00 |
| 49. | Khadija | 500,000.00 |
| 50. | Jackline | 40,000.00 |
| 51. | Zubeda | 100,000.00 |
| 52. | Kelvin | 250,000.00 |
| 53. | Antony | 180,000.00 |
| 54. | Stanley | 3,500,000.00 |
| 55. | Kelvin | 250,000.00 |
| 56. | | 2,000,000.00 |
| 57 | | 220,000.00 |
| 58. | | 4,447,406.00 |
| 59. | | 2,000,000.00 |
| 60. | | 5,000,000.00 |
| 61. | | 1,566,355.00 |

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**

# ‘USAID mshirika muhimu Tanzania safari ya maendeleo kuelekea kipato cha kati’

**Na Craig Hart**

KWA zaidi ya miongo sita, Marekani, kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imekuwa mshirika muhimu wa Tanzania, katika safari yake ya maendeleo kuelekea hadhi ya kipato cha kati na katika kuongeza wastani wa umri wa kuishi kwa miaka 16 katika miongo miwili iliyopita.

Marekani itaendelea kusaidia kudumisha mafanikio haya na mengine, pamoja na kuboresha afya na ustawi wa Tanzania.

Kama Mkurugenzi Mkazi wa USAID nchini Tanzania, najivunia kila siku kuona kazi za wafanyakazi wetu wote wakiwamo Wamarekani na Watanzania pamoja na washirika wanaotekeleza miradi yetu.

Pia nafurahishwa na ushirikiano tuliojenga na sekta binafsi. Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi na kuwawezesha wajasiriamali wa Kitanzania, ni muhimu katika kufikia maendeleo ya kiuchumi endelevu na jumuishi ambayo Watanzania wanastahili na kuyatarajia.

Mwaka uliopita pekee, USAID imetoa zaidi ya dola milioni 400 kama ruzuku ili kuimarisha biashara, kukuza ajira na kuchochea maendeleo nchini Tanzania.

Nataka kusisitiza jambo hili fedha hizi ni ruzuku na sio mikopo; maana yake zimesaidia kuboresha afya, ustawi na kukuza fursa nchini Tanzania bila kuongeza mzigo wa deni la taifa kwa vizazi vijavyo.

Aidha, Shirika la Fedha za Maendeleo la Marekani (DFC) hivi karibuni lilitangaza mkopo wa moja kwa moja wa zaidi ya dola milioni 300 kwa Benki ya CRDB, ambao utawezesha zaidi ya biashara ndogo 4,500 kupata mikopo.

Pamoja na uwezekano wa Tanzania kurejeshwa kwenye mpango wa ushirikiano kupitia Shirika la Changamoto ya Milenia la Marekani (MCC) na mipango mingine ya kiuchumi ya Marekani, mipango hii inaonyesha kujitolea kwa kina kwa Marekani katika kuwawezesha watu wa Tanzania na kuimarisha uchumi wa taifa.

Ushirikiano wa awali wa USAID umepata matokeo makubwa na sekta binafsi ya Tanzania, lakini ili kupata mafanikio makubwa zaidi hapana budi kusaidia biashara binafsi na wajasiriamali wa Kitanzania kuwa washirika katika maendeleo.

Huu ndio ushirikiano utakaoleta matokeo ya kiuchumi ambayo kwa kiasi kikubwa yatazidi kile ambacho USAID na Marekani wanatoa kwa sasa kupitia ufadhili wa maendeleo.



Mkurugenzi Mkazi wa USAID/Tanzania, Craig Hart.

Tunajivunia kuona Prakseda Melkior, mkulima kutoka Morogoro, ambaye alitumia mafunzo aliopata kupitia USAID kukuza biashara yake, kupanua shamba lake, na kuongeza faida, akiendelea kufundisha wakulima wengine zaidi ya 650 wanaofuata nyayo zake.

Rita Sekilovele, ni mnufaika mwingine ambaye alitumia ruzuku kutoka USAID kupanua biashara yake ya uzalishaji wa unga wa mahindi.

Leo, kampuni yake, Super Seki, ni maarufu ikidhihirisha jinsi ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi unavyobadilisha maisha ya wanawake katika sekta ya kilimo nchini Tanzania.

Sasa, jiulize mafanikio ambayo Tanzania ingeweza kupata kukiwa na masoko ya uhakika na washirika wengi wa ujasiriamali kama Prakseda na Rita.

Kupitia USAID, Marekani imedhamiria kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanaweza kukuza biashara zao na kuwainua wengine. Ili kufikia lengo hili, tumeshirikiana tena na DFC kutoa dhamana za mikopo za ziada za dola milioni 52 kwa benki za Amana na CRDB.

Hii itapanua kwa kiasi kikubwa mikopo katika sekta muhimu, ikiwa ni pamoja na uchumi katika sekta zisizo rasmi.

Kati ya fedha hizi, dola milioni 34 zitalenga elimu na sekta isiyo rasmi, dola milioni 10 zitaelekezwa kwenye kilimo, biashara zinazomilikiwa na wanawake, na vijana, na dola milioni 8.8 zitaelekezwa katika sekta ya afya ili kuendeleza biashara na kukuza ushirikiano zaidi nchini Tanzania.

Ikiwa asilimia 75 ya idadi ya Watanzania wako chini ya umri wa miaka 35, na zaidi ya nusu ikiwa ni wanawake, mafanikio ya Tanzania yanategemea mafanikio ya vijana wake.

Ndio maana tunawaweka vijana kuwa wa kipaumbele katika mipango yetu na ndio sababu tumedhamiria kupanua fursa kwa vijana wa Tanzania. Hivi karibuni USAID ilitoa ruzuku 160 kwa biashara za kilimo zinazoongozwa na vijana ili waweze kujipatia zana muhimu kama vile pampu za maji za jua, mashine za usindikaji chakula, na kivuli cha greenhouse. USAID pia ilitoa zaidi ya dola milioni 14 kwa biashara ndogo na za kati ili kukuza ajira.

Mipango hii inatarajiwa kuzalisha karibu dola milioni 43 katika mauzo mapya, ikiwamo asali na korosho kutoka Tanzania hadi nguo, na kutoa zaidi ya ajira 2,000 kwa Watanzania.

Mpango wa Sheria ya Marekani ya Ukuaji na Fursa wa Afrika (AGOA), ulioanzishwa mwaka 2000 na sasa unaotarajia kuendelezwa, unaziondolea biashara za Kitanzania ushuru wa kodi kwa bidhaa zinazouzwa nchini Marekani.

Lengo la AGOA ni kutengeneza uhusiano wa biashara na mahusiano binafsi kati ya nchi zetu mbili kwa njia ambayo zote zinafaidika.

USAID inafanya kazi na Wizara ya Viwanda na Biashara kupanua uelewa wa malengo ya AGOA na kusaidia kampuni zinazotaka kusafirisha bidhaa kwenda Marekani.

Baba wa Taifa, Mwl. Julius Nyerere, alisisitiza kwamba jamii yenye afya ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi.

Kwa miongo kadhaa USAID, pamoja na mashirika mengine ya serikali ya Marekani, yamewekeza mabilioni ya dola katika kuimarisha mifumo ya afya nchini Tanzania. Kupitia ushirikiano na sekta binafsi, tumeanzisha suluhisho bunifu kutatua baadhi ya changamoto kuu.

Mpango huu umepunguza vifo vya kinamama na watoto wachanga kwa asilimia 25 katika maeneo yaliyolengwa. USAID inafanya kazi na sekta binafsi katika sekta zote, ili kufikia maslahi ya pamoja, kama vile kuwapa vijana wasio katika mfumo wa shule ujuzi wa ufundi na mafunzo katika sekta binafsi na umma, na hivyo kuwapa kizazi kijacho cha Watanzania zana na ujuzi ili wafanikiwe.

Ili biashara za Kitanzania zikue, zinahitaji mazingira salama na wezeshi ya biashara. Kuweza kuvuna faida za uwekezaji kunahitaji kuweka nia ya kukuza uwazi, maboresho ya mifumo ya masoko, uhuru wa kisiasa na kukabiliana na ufisadi.

Ninapozungumza na kampuni za Kitanzania na kimataifa zinazovutiwa na kuwekeza nchini Tanzania, wanasisitiza umuhimu wa utawala bora, uwazi, na sheria inayofuatwa kwa usawa, ikiwa ni pamoja na sera za ushuru za haki na kuunda uwanja wa mashindano ulio sawa na wa haki. Mwisho wa siku, serikali zinazolinda haki za kisiasa na kiraia zinavutia mtiririko endelevu wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. USAID inafanya kazi pamoja na taasisi za Kitanzania ili kuweka mazingira rafiki ya biashara ambayo yanawawezesha kupanua biashara, kuwa na ubunifu na muhimu zaidi, kutengeneza ajira na fursa kwa vijana na wanawake wa Kitanzania.

USAID imedhamiria kuimarisha ushirikiano huu sasa na kwa vizazi vijavyo, bega kwa bega na wajasiriamali kama Prakseda na Rita na mamilioni kama wao, ili kutafuta suluhisho zenye faida, haki, na endelevu kwa changamoto za maendeleo.

## Silaa ataka watumishi kutanguliza maslahi ya nchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, amewataka watumishi mkoani Singida kutanguliza maslahi mbele ya wananchi katika utendaji wao kazi, ili kuupaisha mkoa huo na taifa kimaendeleo.

Akizungumza na watumishi wa sekretarieti ya Mkoa wa Singida juzi, alisema iwapo watatanguliza maslahi ya wananchi kazi zitakwenda vizuri.

“Tukiweka maslahi ya hapa Singida mbele kazi zitakwenda vizuri na tutaendelea kujenga taifa letu, niendelee kutoa wito tuchape kazi kwa kasi zaidi na pia tuyatangaze maendeleo makubwa yanayofanywa na serikali ili wananchi wayafahamu,” alisema.

Aidha, alisema katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya serikali imeleta fedha nyingi za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na ni jukumu la watendaji kusimamia fedha hizo, ili iweze kukamilika kwa wakati na ubora unaolingana na thamani ya fedha.

“Rais hajaleta fedha hizi kuja kukaa kwenye akaunti hakikisheni fedha zilizoletwa zinatumika kwenye miradi na msimamie miradi hiyo,” alisema.

Akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Puma, aliwataka kuzingatia masomo kwa kuwa serikali imewajengea shule nzuri zenye mazingira mazuri ya kusoma.

“Sisi tunaoongea hapa shule tulizosoma hazikuwa katika mazingira mazuri, lakini leo hii sisi ni viongozi, nawaomba someni sana serikali inawapenda sana ndio maana imejenga shule nzuri ili msome,” alisema.

Akiwa katika kiwanda cha mafuta ya alizeti cha Wild Flower Grains & Oil Mill Company Limited kilichoko Manispaa ya Singida, alisema ni wakati sasa wa Tanzania kupunguza kuagiza bidhaa nje ya nchi kwa kuwa maendeleo ya viwanda yatarahisisha uchakataji na upatikanaji wa bidhaa mbalimbali ikiwamo mafuta ya kupikia.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, aliwakaribisha wawekezaji kuwekeza katika mkoa huo akisema ni mahali salama na upatikanaji wa umeme na mazao ya biashara kama alizeti na vitunguu.





# Manyara wajipanga kwa kilimo cha alizeti

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara unatarajia kuvuna tani 210,169 za zao la alizeti katika msimu ujao wa kilimo.

Kwa mujibu wa Ofisa Kilimo wa Mkoa huo, Samwel Dahaye, mavuno hayo yatakayopatikana kwenye mashamba yenye ukubwa wa hekta 144,172 na kusaidia kuinua kipato cha wakulima kutokana na bei ya mafuta kupanda na mashudu kuuzwa kwa wingi nje ya nchi.

Dahaye, alisema alizeti ni miongoni mwa mazao ya biashara yanayopewa kipaumbele na wakulima wa mkoa huo.Alisema msimu huu ambao Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA), ilitangaza kuwa na mvua chini ya wastani, wakulima wakiwa makini, zao hilo litawainua kiuchumi.

"Hili zao halihitaji mvua nyingi, wakulima wakijipanga vizuri wakafuata kanuni za kilimo litawatoa, kwa sasa alizeti ina bei, inauzwa nje ya nchi," alisema Dahaye.

Katika hatua nyingine, Katibu Mtendaji wa Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti Manyara (MASUPA), Julian Kambayta, akizungumzia msimu ujao, alisema wameanza kugawa mbegu kwa wakulima ambao ni wanachama wao.

Kambayta, alisema wanagawa mbegu za kisasa kwa wakulima 40 ambao kila mmoja atapanda kwenye shamba la ekari.

"Mbegu hatuwapi bure ila wakulima wanalipa asilimia 90 inabaki asilimia 10, ambayo watalipa wakivuna mfano mbegu ya Sh. 50,000 wanalipia Sh. 45,000 nyingine wakivuna," alisema.

Katibu huyo, alieleza kuwa kila mkulima akilima ekari mbili, watakuwa na ekari 80 zitakazozalisha tani 88,000 sawa na kila ekari kuzalisha tani 1.1 yaani tani 1,100 kwa ekari.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Manyara cha Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Yuda Sulley, alisema wanajipanga kufufua kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti ili kuwahakikishia wanachama wao upatikanaji wa soko la zao hilo.

# Anglikana yataka viongozi wenye hofu ya Mungu

**Na Steven William,** MUHEZA

ASKOFU Mkuu wa Anglikana nchini, Maimbo Mndolwa, amesema kanisa hilo litatumia maadhimisho ya miaka 100 ya kumbukizi ya kifo cha Hayati, Askofu Frank Weston kuhamasisha wananchi kuchagua viongozi wenye hofu ya Mungu katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi ujao.

Akizungumzia kumbukizi hiyo, Askofu Mndolwa, alisema kilele chake kitafanyika Novemba 17, mwaka huu katika Kanisa la Msalaba Mtakatifu Magila Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga.

Alisema maadhimisho hayo yatatanguliwa na matembezi ya safari ya njia ya msalaba, kuanzia Msitu wa Hifadhi wa Nilo hadi Magila-Msalabani.

"Tunamkumbuka Askofu Frank Weston kwa kuwa ndiye mwanzilishi wa Chama cha Skauti Tanzania, chombo ambacho aliona ni vyema kifanye kazi ya kuwaimarisha vijana ambao walikuwa goigoi alipokuwa akiongozana nao katika safari wakati wa vita vya kwanza vya dunia," alisema.

Askofu Weston, pia ndiye mwasisi wa kinachoitwa sasa Mamlaka ya Mafunzo ya Elimu na Ufundi Stadi (VETA) Tanzania.

Kwa mujibu wa Askofu Mndolwa, maadhimisho hayo yatahudhuriwa na wageni kutoka Marekani, Uingereza, Zambia na Dayosisi za Anglikana nchini.

Kumbukizi ya Askofu Weston itafanyika Kanisa la Msalaba Mtakatifu Magila Muheza, mahali alipozikwa 1924.

Askofu Weston, aliyekuwa kiongozi wa kwanza wa Dayosisi ya Zanzibar na Tanga, alizaliwa Septemba 13, mwaka 1817 London Uingereza na kufariki dunia Novemba 2, mwaka 1924 katika nyumba ya uaskofu iliyokuwa Mlima Hegongo Magila-Msalabani Wilaya ya Muheza.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akifurahia jambo baada ya kukabidhiwa zawadi ya mikungu ya ndizi na wanawake wa jukwaa la uwezeshaji kiuchumi Kata ya Kwabada, wilayani Muheza, mkoani Tanga mapema wiki hii. Wengine ni Mkuu wa Mkoa huo, Batilda Buriani (wa tatu kushoto), Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Fani Mussa (kushoto), Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Erasto Mhina (wa pili kushoto), Mkuu wa wilaya hiyo, Zainab Abdallah (wa tatu kulia) na (wa pili kulia) ni Diwani wa Kata ya Kwabada, Victoria Mgimba. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanawake wavunja rekodi serikali mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAWAKE wanane wakazi wa Mtaa wa Mwereni, Kata ya Ngangamfumuni Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wameweka rekodi pekee ya kuwa na idadi kubwa ya wanawake waliojitokeza kwenye eneo moja kuomba nafasi za juu za uongozi wa serikali za mitaa, unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu.

Akizungumza katika kikao kazi cha wadau wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO linalofadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT), mwenyekiti wa mtaa huo kabla ya kumaliza muda wake na kurejeshwa tena katika kura za maoni kutetea kiti hicho, Dyness Minja, alisema na wenzake ni sehemu ya waliokubali kubeba ajenda za wanawake na kuwa sauti ya wote katika vyombo vya maamuzi.

"Uongozi bora wa mwenyekiti wa mtaa, kijiji au kitongoji, ni rasilimali muhimu ya kuchochea maendeleo kwa sababu yeye ndiye mwakilishi wa wananchi katika Baraza la Maendeleo ya Kata (WDC), ngazi ambayo vipaumbele vya bajeti ya halmashauri na taifa vinaanzia kupangwa.

"Ndio maana mimi na wanawake wenzangu katika Mtaa wa Mwereni, tumejitosa kuomba nafasi mbalimbali na kubeba ajenda za wanawake na jamii ili kushughulikia changamoto zinazotukumba," alisema Dyness.

Awali, Mwenyekiti wa Kikundi cha Free Zone Women Group, Catherine Kusaga, akizungumza katika kikao kazi hicho, alisema Dyness amekuwa chachu ya wanawake kuanzisha vikundi vya kiuchumi, vikundi vya kusaidiana na vikoba katika mtaa huo, ndio maana wanawake wameamua kuwatuma kubeba ajenda zao kwenye serikali za mitaa, vijiji na vitongoji.

Mtaa huo, unakabiliwa na changamoto za ukatili wa kijinsia, ikiwamo ubakaji, ulawiti na kunajisi watoto.

Awali, Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, Veronica Ollomi, alisema lengo la mradi huo ni kuwahamasisha wanawake wenye sifa, nia na kiu ya kutamani kuwaongoza wengine kushiriki katika mchakato wa kugombea uongozi.

Kwa mujibu wa Veronica, wanawake wamekuwa wakipiga kelele wanatamani haki zao, usawa, lakini je, wanazo taarifa sahihi za kutamani huo usawa, au je, wakipewa hizo fursa, wanazitumia kama haki zao za msingi.

Kata zinazoguswa na mradi huo ni Pasua na Ngangamfumuni za Manispaa ya Moshi, Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.





# Mume adaiwa kuua mke kwa kipigo kisa wivu wa mapenzi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKAZI wa Mtaa wa Mtakuja Kata ya Kiloleni Manispaa ya Tabora mkoani hapa, Hawa Juma (35) amefariki dunia baada ya kudaiwa kupigwa na mumewe, maarufu Chura (35) kutokana na wivu wa mapenzi.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa huo, Dionis Paul, alisema kuwa tukio hilo lilitokea juzi kwenye nyumba waliyopanga.

Dionis, alisema wana ndoa hao wanadaiwa kuwa na ugomvi kwa muda mrefu na walikuwa wakishtakiana kwake mara mara na kusuluhishwa.

Alisema baada ya kupata taarifa za mauaji hayo kutoka kwa wapangaji wenzao, alikwenda mpaka kwenye eneo la tukio na kuukuta mwili wa mwanamke huyo ukiwa chini chumbani mwao.

Alisema katika chumba hicho, alikuta fimbo, mwiko na mwili huo ukiwa na majeraha kichwani na mguu wa kushoto.

Jirani na rafiki wa marehemu ambaye alikuwa mfanyakazi mwenzake wa kusomba taka, Hawa Juma, alieleza kusikitishwa na tukio hilo na kuiomba serikali kuchukua hatua kali dhidi ya mtuhumiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo yaliyosababishwa na mwanamke huyo kupigwa na kitu butu kichwani na kuvunjwa mguu wa kushoto.

Abwao, alisema chanjo cha ugomvi huo ulioanza usiku wa kuamkia juzi wivu wa mapenzi na mtuhumiwa huyo kudaiwa kumuua mkewe asubuhi.

Alisema baada ya mtuhumiwa kutekeleza tukio hilo alikimbilia kusikojulikana na kwamba jeshi hilo linaendelea kumsaka kwa kushirikiana na wananchi ili akamatwe na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka.



Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM tawi la Kijiji cha Buira, Kata ya Bukumi, Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, Japhet Nyambea, akizungumza na wanachama waliowania uongozi wa vitongoji na kijiji, wakati wa kujaza fomu za kuomba nafasi hizo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakabidhiwa pikipiki

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Edrward Gowele, amekabidhi pikipiki saba kwa viongozi wa idara ya maji ili kuwawezesha kutoa huduma kwa wananchi vijijini.

Pikipiki hizo zimetolewa kwa ajili ya wakuu wa vituo hivyo vya Sirari, Nyamongo,

Ingwe, Kiribo, Gisangura Nyandoto na Kenyamanyori.

Akikabidhi pikipiki hizo, Gowele aliwaonya viongozi kutumia kwa lengo la kusaidia kufikia dhana ya kumtua mama ndoo kichwani badala ya kusafirisha bidhaa za magendo na abiria (bodaboda).

"Kwa yeyote atakayebainika kukiuka matumizi yaliyolengwa atachukuliwa hatua kali za kisheria, hakikisheni mnazitumia kufikia malengo ya kumtua mama ndoo kichwani," alisema.

Kaimu Meneja wa RUWASA Tarime, Pasian John, alisema pikipiki hizo zimenunuliwa kwa Sh. milioni 21 na kusambazwa vijijini katika vituo vya huduma za maji.

"Tunazigawa kwa vituo sita na moja itabaki hapa ofisini kwa ajili ya shughuli za ofisi na kufuatilia huduma katika vituo hivyo na kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi," alisema John.

## Wajasiriamali rasmi mitandao ya kijamii

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

ZAIDI ya wajasiriamali wadogo 200 jijini hapa wanatarajia kuongeza wateja na kipato baada ya kupatiwa mbinu za kileo za kutumia mitandao ya kijamii kunadi bidhaa zao, imefahamika.

Ni baada ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Mwanza kuwapatia mafunzo ya kutumia mitandao hiyo kama sehemu ya kupata masoko na kuondokana na njia asilia ambazo wanazitumia kwa sasa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa Mkuu wa CBE, Profesa Edda Lwoga alisema kuwa wajasiriamali hao ni kutoka masoko ya Kilileli, Buswelu na Kirumba.

Kwa mujibu wa Profesa Lwoga, kupitia Kampasi ya Mwanza, wamewajengea uwezo wajasiriamali hao kuhimili biashara zao, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa dhima ya kuanzishwa kwa chuo hicho ya kutoa elimu ya biashara, kufanya utafiti eneo la biashara, kutoa ushauri wa kitaalamu na kuwajengea uwezo wafanyabiashara, wajasiriamali wadogo, wakati na wakubwa.

"Mwaka 2023/24 tuliwajengea uwezo wajasiriamali 600 kwenye vyuo vyetu. Wajasiriamali wadogo na wakati ni sekta ambayo inahitaji sana elimu hasa wanawake na vijana na wenye ulemavu, hivyo tumejikita zaidi kwenye eneo hilo na sekta ya bodaboda," alisisitiza mkuu huyo wa CBE.

Mkurugenzi wa CBE wa Kampasi hiyo, Dk. Robeth Mashenene, alisema mwaka jana walifanya utafiti katika biashara ya samaki ambao ulilenga kufahamu mbinu za masoko zinazotumika.

Dk. Mashenene, alisema katika utafiti huo, walibaini bado wafanyabiashara wa kitoweo hicho wanatumia njia asilia kwenye masoko badala ya mbinu za kileo kupata wateja.

## Bodaboda, bajaji watangaziwa kiama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KIKOSI cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga kimetangaza msako dhidi ya wamiliki na madereva husani wa pikipiki na bajaji waliondoa namba za usajili na kuandika majina yao kinyume na sheria.

Mkuu wa Kikosi hicho, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP), Florah Nangawe, alitangaza msako huo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake walivyojipanga kuhakikisha wanadhibiti waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda wanaondoa namba za usajili na kuweka majina yao.

ASP Frolah, alisema kila chombo cha usafiri kinatakiwa kuingia barabarani kikiwa kimesajiliwa kwa kuwa na namba za usajili mbele na nyuma.

Alisema madereva na wamiliki watakaokamatwa wakikiuka utaratibu huo, watakamatwa na kuchukuliwa hatua kali, ikiwamo kutozwa faini ya Sh. 10,000 kwa pikipiki, bajaji, magari madogo na makubwa Sh.30,000. Nangawe aliwataka viongozi wa vyama vya waendesha pikipiki na bajaji kuwabana wanachama wao kuacha kutoa namba za usajili na kuweka majina yao, la sivyo watakumbana na mkono wa dola.

Alisema kwa wale ambao makosa yao yatajirudia zaidi ya mara tatu, wataandaliwa mashtaka na kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

## RUWASA yapewa gari

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoani Shinyanga na Mara imekabidhiwa gari kwa ajili ya kuwawezesha watumishi wake kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi.

Akikabidhi gari hilo, Mkuu wa Mkoa huo, Anamringi Macha, aliutaka wakala huo kulitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na kulitunza.

Alisema serikali imetoa kitendea kazi hicho ili kikatumike kwa shughuli za serikali na kukagua miradi ya maji ambayo inatekelezwa kwa wananchi.

Meneja wa RUWASA wa mkoa huo, Mhandisi Julieth Payovela, alisema gari hilo litakwenda kuongeza ufanisi wa utendaji wao wa kazi, kusimamia miradi ya maji ili iwe na kiwango chenye ubora na kukamilika kwa wakati.

ama
AFYA NA MAZINGIRA
ALHAMISI OKTOBA 31, 2024



Ukurasa 12

**Nje na ndani mpox: Ilikotokea, dalili, tiba, chanjo, shida ngono**



**MAGEUZI ARDHI YA KILIMO... Wanachuo waja na ubunifu ndani ya tabianchi**

Ukurasa 14

# Msalaba Mwekundu yawekeza wataalamu mipakani kukabili hatari ya Mpox kuingia

**Na Sabato Kasika**

UGONJWA wa Mpox unaotisha jamii katika mtazamo mpya, nchi jirani na kwingineko maradhi hayo yamefika, ziko katika hatua ya kujihami, hali kadhalika Shirika la Afya Duniani (WHO) liko katika jitihada za vita hivyo.

Nchini, Chama cha Msalaba Mwekundu tawi la Tanzania, sasa kimejipanga kuhakikisha ugonjwa mpox hauingii nchini. Ni hatua inayohusika na kusambaza wafanyakazi 750 wa kujitolea katika mikoa ya mipakani, ambao wanatoa elimu kwa wananchi na mbinu za kuutambua ugonjwa huo, hata kuuepuka.

Baadhi ya mikoa wafanyakazi hao wamepelekwa ni Mara, Mwanza, Kagera, Kigoma, Rukwa, Katavi, Songwe, Mbeya na Ruvuma ambazo ziko jirani na nchi nyinginezo.

Utaratibu wao wanatembelea nyumba, kwenye mikusanyiko ya watu, vyombo vya usafiri, vituo vya mabasi na maeneo mengine kutoa elimu.

Lengo ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa kuhusu ugonjwa huo, ikiwamo dalili zake na jinsi mtu anaweza kuuepuka au hata anapoipata, asisambaze kwa wengine.

Meneja wa Kukabiliana na Maafa wa chama hicho, Samwel Katamba, anasema mikakati hiyo, imeonyesha kusaidia kwa kiasi kikubwa, hakuna waliokutwa na ugonjwa huo.

"Vijana wetu wanatoa elimu ya mtu kutambua dalili za ugonjwa huo, jinsi ya kujikinga na hata kupata matibabu kwa kushirikiana na watu wa huduma ya afya ngazi ya jamii," anasema Katamba.




Ziara ya aliyekuwa Katibu Mkuu, Dk. Zainab Chaula, katika wizara yenye dhamana na afya mwaka 2020, alipozuru mpaka wa Mutukula, Kagera unaotenganisha Tanzania na Uganda, kukagua utayari wao kukabili magonjwa ya mlipuko. Ilikuwa kabla ya Mpox. **PICHA: MAKTABA.**

Ana ufafanuzi kwamba, Tanzania imepakana na baadhi ya nchi zenye changamoto ya magonjwa ya mlipuko ukiwamo mpox, hivyo wameona washirikiane na serikali kukabiliana na ugonjwa huo, kwa kupeleka watalamu hao 750.

"Wizara ya Afya inasema ugonjwa huo haujaingia nchini, lakini suala la kuchukua tahadhari ni muhimu, ndio maana tumeweka wafanyakazi wetu wa kujitolea wasaidie kuelimisha jamii ili iwe uelewa wa kutosha na kuchukua tahadhari," anasema.

Ofisa wa Maafa wa chama hicho, Christa Chrisstian, anataja majukumu ya Msalaba Mwekundu ni kukabili majanga na kwamba mlipuko wa Mpox uko katika orodha hiyo, janga linalohitaji kukabiliwa.

"Tunashirikiana na Wizara ya Afya katika vita hii, ndio maana kuna vijana wetu pamoja na watoa huduma ya afya ngazi ya jamii ambao ni wa serikali," anasema Christa.

Mtaalamu wa Saikolojia wa chama hicho, Maudline Tarazo, anasema watu wanapokumbwa na majanga au magonjwa, wengine hukata tamaa, akifafanua kuwa watu wa aina hiyo wanahitaji kuwekwa sawa.

"Vijana wetu wanaoendelea kusaidia jamii huko kwenye mikoa ya mipakani, wapo ambao ni wataalamu wa saikolojia, wanaosaidia kuwaweka watu sawa, ili hata kama kwa bahati mbaya ugonjwa ukafika maeneo hayo, wakabiliane nao bila hofu," anasema Maudline.

Aidha, anasema wananchi wameelekezwa kupiga simu namba 0800750150 inayopigwa bure, iwapo watahisi dalili za ugonjwa huo, ili hatua zichukuliwe haraka.

Maudline anasema, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania kina wataalamu wa fani nyingi zinazohitajika wakati wa majanga kama ya ajali, mafuriko, magonjwa, ukame na kimbunga.

**MTANZANIA ALIYEGUNDULIKA**

Wiki mbili zilizopita, Wizara ya Afya ilithibitisha kisa cha kwanza Mtanzania, kubainika amepata maambukizi ya Mpox, il;a akahakikisha nchi iko salama dhidi ya maradhi mpox.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Roida Andusamile, anasema Mtanzania huyo anayekadiriwa kuwa na miaka 32, alibainika kuwa na ugonjwa huo akiwa nchini Zambia.

Katika taarifa yake aliyoitoa kwa umma Oktoba 11 mwaka huu, Roida anasema walipata taarifa tukio hilo kutoka serikali ya Zambia kuwa Mtanzania huyo alivuka mpaka kwenda nchini humo mwanzoni mwa mwezi uliopita kupitia mpaka wa Tunduma, kuingia Nakonde, mnamo Septemba 2, mwaka huu.

Inaelezwa kuwa wakati anavuka, hakuwa na dalili zozote za ugonjwa huo, lakini mwezi mmoja baadaye akiwa nchini humo alikwenda katika kliniki na kupata matibabu ya awali.

Roida anasema mgonjwa huyo alichukuliwa vipimo mwanzoni mwa Oktoba ambavyo vilithibitisha kuwa ana maambukizi ya ugonjwa huo na kuanza kupewa matibabu.

Dalili za ugonjwa mpox inatajwa huweza kuonekana kati ya siku tatu hadi 21 tangu kuambukizwa, hivyo Mtanzania huyo alianza kuonyesha dalili mwezi mmoja baada ya kutoka nchini.

Aidha, Wizara ya Afya imewahakikishia kuwa, bado Tanzania iko salama na hakuna mgonjwa wa mpox aliyebainika nchini hadi

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Nje na ndani mpox: Ilikotokea, dalili, tiba, chanjo, shida ngono



Hali halisi ya mwathiriwa wa mpox. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

AINA mpya ya virusi vya mpox inaenea kwa haraka katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na wataalamu wanasema ni hatari zaidi waliyoishuhudia.

Mpox, ambayo zamani iliitwa monkey pox, imeenea katika sehemu za magharibi na kati mwa Afrika na kesi zimekuwa zikiongezeka katika bara hilo kwa miongo kadhaa.

Mnamo mwaka 2022, ikawa janga la ulimwengu likiathiri Ulaya, Australia, Marekani na nchi nyingine nyingi.

Ugonjwa huo husababishwa na virusi hivyo - monkeypox vinavyopatikana katika kundi moja la virusi na ndui, ingawa inatajwa si kali sana.

Ni maradhi yaliyoonekana tangu zama za miaka 1950. Inatajwa virusi hivyo awali vilisambazwa kutoka kwa wanyama hadi wanadamu na hupatikana zaidi katika nchi zilizo karibu na misitu ya kitropiki.

Katika maeneo hayo, kunatajwa kuwapo magonjwa na vifo, kukitajwa waathirika wakuu ni watoto wenyue umri chini ya miaka 15.

Hapo kuna aina mbili kuu za virusi. Ya kwanza inatajwa kusababisha mlipuko kimataifa na mnamo 2022, ulienea kwa takriban nchi 100, ambazo hazikuwahi kukumbwa na virusi hivyo.

Pia, kuna shida ya virusi vya pili, kwamba ni hatari zaidi na vya kawaida katika Afrika ya Kati, ndio vilivyogunduliwa hivi karibuni nchini DRC.

Aina hizo mbili, zinatajwa kubeba hatari tofauti za ugonjwa huo hadi kufikia vifo.

**DALILI ZAKE**

Kunatajwa dalili za awali, zinajumuisha homa, maumivu ya kichwa, uvimbe, maumivu ya mgongo na misuli kuuma.

Mara baada ya kuwapo homa hiyo, inaelezwa upele unaweza kutokea na mara nyingi huanza kwenye uso, kisha kuenea sehemu nyinginezo za mwili, mara nyingi viganja vya mikono na nyayo za miguu.

Ni upele unaoweza ama kuwasha au kumuuumiza mtu na unabadilika kupitia hatua tofauti, kabla na hatimaye kutimia kutengeneza kipele, ambacho hutumbuka baadaye.

Vidonda vyake vinatajwa kuweza kusababisha makovu na maambukizi kawaida huisha yenyewe na hudumu kati ya siku 14 na 21.

Wapo ambao huwatokea vidonda vinawashambulia mwili mzima, na hasa mdomoni, machoni na sehemu za siri.

**INAVYOENEA MWILINI**

Ugonjwa mpox huenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, asiyeumwa anapokuwa karibu na aliyeambukizwa, ikiwa ni pamoja na kupitia ngono, kugusana ngozi na kuzungumza au kupumua karibu.

Virusi vyake vinaweza kuingia mwilini kupitia ngozi iliyo na michubuko, njia ya kupumua au macho na mdomo.

Inaweza pia kuenea kwa kugusa vitu ambavyo ama vilishikwa au kutumiwa na mwenye virusi, kama vile matandiko, nguo na taulo.

Njia nyinginezi zinahusu kugusana kwa karibu na wanyama walioambukizwa kama vile nyani na panya.

Wakati wa mlipuko wa kimataifa uliotokea mwaka 2022, virusi hivyo vilienea zaidi kupitia ngono na ndio chanzo kimojwapo kinatajwa kuchangia maradhi hayo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mawasiliano ya ngono yakichukua nafasi, ingwa maambukizi yake yameanzia jamii nyingine.

**ALIYE HATARINI**

mara nyingi inatajwa kupatikana kwa watu wanaofanya ngono mwanaume dhidi ya mwanaume.

Hata hivyo, katika ujkumla inatajwa kuwa mtu ambaye ana mawasiliano ya karibu na mtu aliye na dalili, anaweza kufikiwa na virusi, hapio ikiwagusa wafanyakazi wa afya na familia zao.

Hivyo, ushauri uliopo sasa ni kuepuka kugusana kwa karibu na mtu yeyote mwenye mpox na kuosha mikono kwa sabuni na maji, ikiwa virusi viko katika jamii yako.

Kwa ambao wana mpox, Shirika la Afya Duniani (WHO), linaelekeza kwamba wanapaswa kujitenga na wengine, hadi vidonda vyao vyote vitoweke, huku waliopona wanapewa tahadhari kuzingatia ngono salama, wiki 12 baada ya kupona.

**SIRI YA TIBA**

Kimsingi, tiba iliyoundwa ka ugonjwa ndui, inaweza pia kuwa muhimu kutibu mpox, lakini kuna utafiti kuhusu manufaa zaidi.

Milipuko ya mpox, unatajwa na WHO unaweza kudhibitiwa kwa kuzuia maambukizi, njia bora ya kufanya hivyo ni kwa chanjo.

Kuna chanjo tatu ambazo zipo, lakinio ni kwa watu walio hatarini tu au ambao wamewasiliana kwa karibu na mtu aliyeambukizwa kwa kawaida wanaweza kuipata.

WHO kwa sasa haipendekezi kuchanja watu wote. Majaribio zaidi ya chanjo dhidi ya aina mpya za mpox yanahitajika ili kuelewa ni kiasi gani cha ulinzi kinachotoa.



# MSALABA MWEKUNDU YAWEKEZA WATAALAMU MIPAKANI KUKABILI HATARI YA MPOX KUINGIA

**Inatoka Uk. 11**

sasa, ikiendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo uliopo kuhusu ugonjwa huo na kutoa taarifa kwa umma. Wito unatolewa na serikali kwa jamii, kuendelea kuzingatia kanuni za usafi, kutopeana mikono na kutoa taarifa kwa kutumia namba 199, kuhakikisha ugonjwa huo haungii na kusambaa nchini.

Tangu kuripotiwa kwenye nchi jirani Agosti mwaka huu, Wizara ya Afya imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuukabili, huku ikiendelea kuwataka Watanzania kuchukua tahadhari.

Serikali kupitia Waziri wa Afya, Jenista, katika maelezo yake kwa wanahabari jijini Dodoma, akasema Tanzania imejipanga kudhibiti mpox usiingie nchini.

Akafafanua kuwa hilo linafanyika kwa kuimarisha uchunguzi kwa wasafiri kupitia huduma za afya mipakani; bandarini, nchi kavu na viwanja vya ndege, kubaini viashiria na hatua stahiki.

Waziri Jenista akasema, Nio hatua inayotokana na uhalisia baada ya tangazo rasmi la WHO, kutoa tahadhari ya afya duniani.

Waziri akahidi kwamba, wizara kwa kushirikiana na wataalamu wa afya nchini, wakajipanga kufuatilia katika jamii, viashiria au daliliza za ugonjwa huo, ili kumhudumia kwa haraka mhusika, ilia kupunguza kusambaa kwake.

Wizara ya Afya, kupitia Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, ikaeleza namna wataalamu wa afya nchini walivyojipanga kutoa huduma za tiba kwa watakaobainika kuwa na mpox.

AFYA

# Wanasheria wa kike wacharuka kuzidi ukatili na ukiukwaji haki za watoto

**Na Beatrice Moses**

KUWAPO matukio ya mauaji na utekaji wa watoto nchini, hata kuripotiwa kwenye vyombo kadhaa vya vya habari, sasa yanawashtua mawakili wanawake kupitia Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), wakiamua kupaza sauti kukemea vitendo hivyo na wanakishauri hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa wahusika.

Makamu wa Rais TLS, Laetitia Ntagazwa, ametamka katika maandamano yao ya amani Oktoba 18 mwaka huu, yaliyolenga kufikisha ujumbe serikalini, taasisi na wadau wa watoto na jamii kwa ujumla.

Wakili Ntagazwa, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya tukio hilo, anasema wameungana siku hiyo kuipazia sauti jamii, kukemea ukatili na mauaji dhidi ya watoto, ubakaji na utekaji.

Kurejea Ripoti ya Jeshi la Polisi Tanzania ya mwaka 2020, inaonyesha ongezeko la asilimia 25.95 la ukatili dhidi ya watoto, kitakwimu kwa mwaka 2020 kulikuwa na matukio 7,388, kutoka matukio 5,803 yaliyoripotiwa mwaka 2015.

Ni mchanganuo anauoueleza kwamba, kila mwezi kuna watoto 616 wanaofanyiwa vitendo vya ukatili.

Pia, kurejea tafiti za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya Mwaka 2023, inaonyesha kuwapo matukio ya kikatili 464, yalifanywa dhidi ya watoto na yakaripotiwa.

Wakili Ntagazwa anabainisha kuwa ripoti ya mwaka 2023, inaonyesha kutoka matukio 350 kwa mwaka 2022, licha ya kuwapo Sheria ya Mtoto Toleo la 2019 inayomlinda mtoto

"Kwa ujumla, waathirika wakubwa wa ukatili na mauaji katika nchi yetu ya Tanzania ni watoto. Ukatili huu dhidi ya watoto una sura mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vitendo vya kumiza mwili kama vile, kipigo, kubakwa, kulawitiwa, kuchomwa moto, kukatwa viungo, kudhalilishwa kingono, kuteswa na hata kuuawa," anasema.

Pia, anataja aina nyingine za ukatili unaomwathiri mtoto kisaikolojia na kukiuka utu wake, akielekezwa na ama wazazi au walezi wake.

Wakili Ntagazwa anarejea hivi karibuni biashara kuna haramu za watu zimekuwa zikishamiri, watoto wakiathirika kikatili, huku taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ikionyesha asilimia 73 ya waathirika mwaka 2022/2023, walikuwa ni watoto.

Taarifa ya ukatili, zinaonyesha kuwa watoto hutendewa, aidha wao kwa wao, au jamii zinazowazunguka, yakitokea maeneo kama nyumbani kwao, shuleni, kwenye ibada, mikusanyiko, vyombo vya usafiri, pia kutoka watu wa karibu wanaowaamini.



Makamu Rais wa Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS), Laetitia Ntagazwa. **PICHA: MAKTABA**

### TAFSIRI YA SHERIA

Umuhimu wake unatajwa kuanzia kuwapo Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na nyingine zinazomlinda.

Pia, inaelezwa haja ya serikali kuona umuhimu kuwa na kitengo maalum cha watoto katika Wizara ya Maendelo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Hiyo inaendana na haja ya kuwapo Dawati la Jinsia na Watoto ndani ya Polisi, pia kuanzishwa kinachoitwa 'Mama Samia Legal Aid Campaign.'

"Hizi zote ni juhudi za serikali katika kupambana dhidi ya vitendo vya ukatili kwa watoto, hata hivyo," anatamka Wakili Ntanagazwa.

Anafafanua pi hatua za kuwapo Kifungu cha Saba cha Sheria ya Makosa ya Jinai ya Mwaka 1966, inayowataka wananchi kutoa taarifa pale sheria inapovunjwa au inapokaribia kuvunjwa.

"Jukumu la kutoa taarifa/kuchukua hatua dhidi ya haki inapovunjwa au karibia kuvunjwa, pia liko kikatiba..." anasema.

Kipengele kingine anachokitaja ni Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2019, inayotoa jukumu la kila mwananchi kumlinda mtoto dhidi ya ukatili.

Aidha, inarejewa Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990 na Mkataba wa Haki za Mtoto wa Mwaka 1989, zinazotoa haki ya asili ya kuishi kwa mtoto na kuzitaka nchi wanachama kuilinda hilo kwa maendeleo ya mtoto kadri inavyowezekana.

"Kwa kuzingatia wajibu huu tulio nao kama wananchi na nchi/serikali yetu kwa ujumla, lakini zaidi kama wanawake wanasheria na wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika chini ya Kifungu cha Nne cha Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika.

"Ni vyema na wakati muafaka sasa tukakumbushana wajibu huu wa kuwalinda watoto dhidi ya ukatili na mauaji kisheria na kutoa ushauri kwa serikali na msaada wa kisheria kwa jamii, kwa kaulimbiu ya Tanzania Salama ni Jukumu la Wote," anaeleza Ntagazwa.

Eneo lingine analotaja ni kuweka na kutunza ushahidi wa ukatilii, mfano mtoto anapobakwa asiogeshwe na nguo kufuliwa, kutunza ushahidi muhimu.

Anaendelea: "Watu wote kuwa doria mitaani kwetu, mtu asiyeeleweka au anayeshukiwa ahojiwe na wananchi na kuripotiwa polisi bila kujichukulia sheria mikononi, kuwasikiliza watoto na kutowadharau wanapoongea jambo hata kama tunahisi la kijinga."

Mtazamo mwingine unafafanua kufundisha ulinzi kwa kutumia teknolojia kama vile kamera za 'CCTV' kupata rekodi za uhalifu katika jamii na kuzuia wahalifu watarajiwa kujiingiza katika ukatili huo kwa watoto.

"Sisi wanasheria wanawake, tunaahidi kuendelea kutoa elimu ya sheria katika jamii zetu kuziwezesha kujua wajibu wake kisheria na kutokomeza vitendo vya kikatili na mauaji kwa watoto," anasema Ntagazwa.

Katika jitihada hizo, anatamka kuiomba polisi kupeleleza vema matukio yote ya ukatili na mauaji kwa watoto, ili kupata ushahidi sahihi.

Hapo kuna ushauri kwamba Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, kuendesha mashauri hayo kwa weledi, pia mahakama kutenda haki kwenye mashauri yote ya ukatili na mauaji ya watoto, huku jamii nayo ikihamasishwa ushirikiano wa ushahidi na taarifa sahihi kwenye mashauri husika mahakamani.

> Matukio haya yanawatesa na kuwapa hofu zaidi wajane, maana wengi hawana uwezo wa kusomesha watoto wao kwenye shule za kwenda na basi maalum.

### RAIS WA TLS

Rais wa TLS, Wakili Boniface Mwabukusi, anaeleza wazazi wanaosusa kujiandikisha kupiga kura, nao wanawatendea ukatili watoto kwa kuwanyima kupata viongozi bora.

Pia, anashauri kuondolewa ombwe la kumtenga mtoto, kwa kuwa wana haki sawa ya kulindwa dhidi ya hatari zote.

Mkurugenzi wa Umoja wa Wajane Tanzania (TAWIA), Rose Sarwatt, anasema utekaji na mauaji siyo utamaduni wa Watanzania, bali huibuka hasa inapokaribia uchaguzi.

Hivyo, anashauri serikali ihakikishe inawasaka wahusika na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria kukomesha vitendo hivyo.

"Matukio haya yanawatesa na kuwapa hofu zaidi wajane, maana wengi hawana uwezo wa kusomesha watoto wao kwenye shule za kwenda na basi maalum.

"Pia, hata kuwa na msaidizi wa kazi za nyumbani ambaye anaweza kusaidia kuangalia watoto, hivyo mjane anajikunyata nyumbani badala ya kujitafutia kipato," anahitimisha Mwambukusi.

MAZINGIRA

## MAGEUZI ARDHI YA KILIMO...

# Wanachuo waja na ubunifu ndani ya tabianchi inayotumika shamba

## •Mashine nazo zaundiwa mapya yake

**Na Grace Mwakalinga**



Shughuli za kilimo zikiendelea shambani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

SEKTA ya Kilimo bado inakabiliwa na changamoto zinazoathiri uzalishaji mazao na uchumi wa wakulima, ikiwamo ukosefu wa vifaa vya kisasa na teknolojia inayowafanya wakulima wasiweze kuongeza uzalishaji.

Wengi bado wanadumu kutumia njia za jadi katika kilimo, zisizotoa matokeo bora, uelewa duni wa teknolojia mpya inaingia katika changamoto nyingine.

Hapo wakulima hawana maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya teknolojia za kisasa kama vile umwagiliaji wa kisasa na mbinu za kilimo endelevu.

Mabadiliko ya tabianchi ni changamoto inayoongezeka, kwa sababu inahusisha mabadiliko ya hali ya hewa yanayoathiri uzalishaji wa mazao na wakulima wengi hawana teknolojia za kukabiliana nayo.

Kukosekana taarifa sahihi kuhusu sekta ya kilimo, kunakwamisha jitihada za wakulima katika kuzalisha mazao yao kwa tija, mifumo duni ya mawasiliano inawafanya wakulima washindwe kupata habari muhimu kufahamu ni wakati gani sahihi wanapaswa kulima.

**MHITIMU ABUNI**

Katika juhudi za kuboresha sekta ya kilimo nchini Tanzania, Radhia Seleman, Mhitimu wa Stashahada ya Uhandisi Umeme kutoka Chuo cha Uhandisi na Teknolojia cha Al- Maktoum (AMCET) kilichoko Dar es Salaam, amevumbua mfumo wa kiteknolojia unaowezesha wakulima, wataalamu na wadau wa kilimo kupata taarifa muhimu kuhusu udongo.

Mfumo huo, unaotumia teknolojia walioibatiza 'Global System for Mobile Communications (GSM), ambao ni wa mawasiliano ya simu za mkononi unaotumika kimataifa, kutoa huduma za sauti na data, ulianzishwa mwishoni mwa miaka ya 1980 na kusambaa kwa kasi duniani kote.

Radhia anasema, teknolojia hiyo inawapa wakulima taarifa kwa njia ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS), ikiwamo kufahamu aina ya mbolea inayofaa, kiwango kinachohitajika cha maji kwenye udongo na aina ya mazao yanayostawi kulingana na udongo wa eneo husika.

"Huu ni mfumo wa kipekee unaowezesha wakulima kupata taarifa sahihi na kwa wakati, hatua hii inayolenga kuongeza uzalishaji na kuboresha ufanisi wa kilimo nchini," anasema Radhia.

Anasema, wakati anaandaa teknolojia hiyo, alifanya uchunguzi kwa kuzingatia vigezo muhimu vya udongo kama vile kipimo cha 'asidi pH' joto na unyevunyevu, akihakikisha mfumo huo una uwezo wa kutuma taarifa kwa 'GSM' na kuonyesha matokeo kwenye skrini.

"Tulifanya mradi huu hapa chuoni kwa lengo la kuboresha kilimo kwa kutumia teknolojia, na nia yetu ni kufanikisha maendeleo zaidi kwenye sekta hii,"anasimulia Radhia, akionyesha matumaini ya kuendelea kuchangia ubunifu unazoweza kuwa na manufaa kwa jamii.

**KAZI ZA MASHINE**

Radhia anasisitiza umuhimu wa kuwa na ushirikiano na ujasiri kwa wanawake katika fani ya teknolojia, akisema anaamini wanaweza kufaulu zaidi ikiwa watajiamini na kuwa na juhudi katika kutekeleza mawazo yao ya kibunifu.

Mbunifu mwingine, Huruma Kimbwanga, mhitimu wa fani ya Uhandisi wa Umeme, ameonyesha ubunifu wa kutengeneza mfumo wa kukamata vitu vyote vyenye asili ya chuma vinavyoweza kujitokeza wakati wa kusaga nafasi kwenye mashine.

Anasema ni mfumo unaotumia teknolojia ya kihisio au maarufu (sensor) kubaini uwapo wa vyuma, unaotoa taarifa za haraka ya kuwapo kwa vifaa hivyo na una uwezo wa kuviondoa kwa ufanisi.

Huruma anaeleza furaha yake kuhusu mafanikio kubuni mfumo huo, akisema amefanikiwa kubuni kitu cha namna hiyo na tayari ameuwasilisha kwa uongozi wa chuo (AMCET) na anaongeza kuwa bado hajafanya maonyesho ya ubunifu katika maeneo mengine, akisubiri utaratibu utakaomruhusu kufanya hivyo.

"Natamani kuwekeza zaidi katika teknolojia hii na kuwa miongoni mwa wabunifu bora duniani, nimeanza na ubunifu huu, lakini nitafanya vitu vingine na vitakuwa vizuri, huu ni mfano wa juhudi za vijana wa Kitanzania katika kutumia ujuzi wao wa kiufundi kuboresha sekta za viwanda na kuongeza ufanisi katika shughuli za uzalishaji," anasema Huruma.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Jannat Sulayman, anaeleza kuwa taasisi hiyo inajivunia kuwafundisha na kuwaandaa wanafunzi kuwa wabunifu wenye uwezo wa kutatua changamoto kwenye jamii.

Katika kufanikisha hayo, chuo kimeanzisha programu inayoitwa 'Ndoto', inayowalenga vijana wanaohitimu kidato cha nne kutoka maeneo mbalimbali nchini, kuwawezesha kuelewa changamoto za jamii zao kwa mtazamo chanya na kuwa sehemu ya utatuzi.

Anasema, utekelezaji wake, wanafunzi wanapewa mafunzo ya miezi mitatu kuhusu jinsi ya kushughulikia changamoto zinazowakabili, ikiwa ni pamoja na kubuni mifumo na vifaa vya kiteknolojia ambavyo vitakuwa msaada katika sekta mbalimbali kama vile afya, maji na nishati.

Anaongeza kuwa, AMCET pia inafanya kazi na wanafunzi kutoka taasisi nyingine kama Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Kote anasema, wanawapa wanaojifunza mafunzo ya vitendo kuhusu ubunifu na teknolojia, ili kuwajengea ujuzi wa kushindana na kufaulu katika masoko ya ajira na ubunifu.

Katika mahafali yake Chuo cha AMCET, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2021, Mkuu wa Chuo, Dk. Hamdun Sulayman, anasisitiza umuhimu wa ubunifu katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

Anaeleza kuwa, AMCET inatoa elimu ya kiwango cha juu inayoowapa wahitimu ujuzi wa vitendo na kuwaandaa kuwa wataalamu na wabunifu wenye uwezo wa kushughulikia masuala ya kijamii kwa weledi na ari.

Dk. Sulayman anaongeza kuwa, chuo hicho pia kina kituo maalum cha ubunifu, kinachowasaidia zaidi ya wanafunzi 300 kuunda mifumo ya kutatua changamoto katika sekta mbalimbali, ikiwamo mfumo wa malipo ya maji kwa njia ya kabla ya matumizi (Pre-Paid Water System).

Anasema kwamba AMCET Innovation Hub mwaka 2023 ilitambuliwa kama "Kiota Bora cha Mwaka" kwa kushinda tuzo ya Africa Fintech and AI Award.

Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema inasaidia mazingira wezeshi kwa maendeleo ya elimu na teknolojia.

Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Adolph Ndunguru, anaeleza kuwa ubunifu wa kiteknolojia unaofanywa na wanafunzi ni muhimu kwa taifa, na wajibu wa serikali ni kuhakikisha wabunifu wanapata masoko ya bidhaa zao.

"Serikali imekuwa ikiwekeza katika mifumo ya elimu ya amali inayolenga kutoa maarifa ya kinadharia na ujuzi wa vitendo ili kuwawezesha wahitimu kujitegemea na kuchangia kikamilifu katika sekta mbalimbali," anasema Ndunguru.

Hadi sasa, ubunifu kama wa Radhia Seleman unatajwa kuwa mfano wa jinsi teknolojia inayoweza kutumiwa kuboresha sekta ya kilimo nchini kwa kuendelea kuwekeza katika elimu na ubunifu.

Ni ushirikiano wa serikali, vyuo na sekta binafsi unahitajika ili Tanzania iendelee kufanya mapinduzi ya kiteknolojia yatakayoboresha sekta ya kilimo, afya na uchumi kwa ujumla.



Kinamama wilayani Ikungi, wakiwa katika mjumuiko wao ndani ya shamba la pamoja.



## Ikungi kuongeza uzalishaji chakula

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WILAYA ya Ikungi mkoani Singida inatarajia kuzalisha tani 402,753.7 za mazao katika msimu mpya wa kilimo wa mwaka 2024/25 na kujitosheleza kwa chakula.

Hayo yamo katika taarifa ya Mkuu wake, Thomas Apson iliyosomwa jana katika kikao cha wadau wa kilimo, viongozi wa vyama vya ushirika, maofisa watendaji, ugani na wakulima wa kata za wilaya hiyo.

Apson katika taarifa hiyo, alisema wilaya hiyo imeweka lengo la kuzalisha tani hizo za chakula kwa msimu huo zaidi ya tani 90,735.8 ilizozalisha mwaka uliopita wa 2023/24.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kwa msimu huu, mikakati kabambe imewekwa kuhakikisha lengo hilo linafikiwa.

"Kila kaya ilime ekari zisizopungua mbili za mazao ya chakula na ekari tatu za mazao ya biashara kama vile alizeti, korosho, dengu na pamba, lengo ni kumfanya mkulima aondokane na tatizo la kiuchumi," alisema.

Ofisa Kilimo wa Wilaya hiyo, Issa Mtweve, aliwaagiza maofisa ugani kuhakikisha kila mkulima anaorodheshwa katika daftari la ruzuku ya mbolea na mbegu.

Alisema maofisa pia wanatakiwa kusaidia kutoa elimu kwa wakulima na kuhakikisha kila mmoja anapeleka udongo wake maabara kupima na kujua afya ya udongo katika shamba lake.

## Wazazi watakiwa kuzingatia lishe bora

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISA Muuguzi Msaidizi wa Kituo cha Afya Makole kilichoko jijini hapo, Christopher Tarimo, amewataka wazazi kuzingatia ulaji bora wa vyakula baada ya kujifungua ili kumkinga mtoto na maradhi ya utapiamlo kutokana na lishe duni.

Tarimo alitoa wito huo jana wakati akitoa elimu ya namna sahihi ya kumnyonyesha mtoto na lishe kwa wajawazito waliojifungua katika wodi ya wazazi ya kituo hicho.

Alisema mtoto anapata chakula kupitia mama, hivyo wazazi wanapaswa kuzingatia ulaji wa vyakula vyenye virutubisho ili kumsaidia mtoto kupata maziwa ya kutosha.

Alisema wazazi wanapopata milo ya asubuhi, mchana na jioni wanatakiwa kuhakikisha ina virutubisho vya kutosha na kupata maziwa ya kutosha wakati wa kunyonyesha.

Ofisa muuguzi huyo, pia alitoa elimu ya unyonyeshaji kwa kinamama waliojifungua ya ukaaji wanaponyonyesha watoto. Alisema ili mtoto anyonye vizuri, anapaswa kushikwa vizuri asipaliwe na kukohoa.

Aliwakumbusha wazazi na walezi wa watoto kuhudhuria kliniki ili kupata elimu ya unyonyeshaji ambayo itawasaidia kujua namna ya kumnyonyesha mtoto.

Alisema wakihudhuria kliniki pia itawasaidia kupata elimu ya utumiaji vyakula ambavyo vitawasaidia wazazi kupata virutubisho.

# Ujenzi madaraja, barabara wapamba moto nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD), Mohamed Besta, amesema serikali inaendelea kutekeleza miradi 77 ya ujenzi wa barabara na madaraja yenye thamani ya Sh. trilioni 4.6.

Besta alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati wa kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya lami ya mzunguko wa nje kipande cha pili chenye kilomita 60.

Alisema tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, ameweka kipaumbele katika ujenzi wa barabara na madaraja ili kurahisisa usafiri na usafirishaji.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi 77 ya ujenzi wa barabara na madaraja yenye thamani ya takribani triloni 4.6.

"Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja inaendelea kwa kasi maeneo mbalimbali nchini na hakuna mradi uliokwama kwasababu Serikali ya Rais Samia imekuwa ikilipa makandarasi kulingana na mikataba," alisema.

Besta, alisema miradi 25 ya ujenzi wa barabara zenye mtandao wa kilomita 1198 na thamani ya Sh. trilioni 1.685 imekamilikwa kwa asilimia 100.

Alisema kwa upande wa daraja Kigogo Busisi la JPM kwa gharama ya Sh. bilioni 717 fedha za walipa kodi, ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 94.

Alisema kutokana na mafanikio ya ujenzi wa miundombionu ya barabara na madaraja, imeifanya Tanzania kushika nafasi ya sita kati ya nchi 54 za Afrika kuwa na mtandao bora wa barabara ikipanda kutoka nafasi ya 16 iliyokuwapo mwaka 2022 kulingana na Takwimu za Statista.com.

Akizungumzia ujenzi wa barabara ya mzunguko lot 2, Besta, alipongeza kasi yake na kumtaka mkandarasi kuhakikisha unakamilika ndani ya muda uliopangwa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akijadiliana jambo na Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango Malecela, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Taasisi za fedha zapewa changamoto

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amezitaka taasisi za fedha kufanya utafiti wa maeneo ya uzalishaji yenye mzunguko mkubwa wa fedha na kupeleka huduma kwa usalama wa wananchi.

Dendego, alitoa wito huo jana kwa viongozi na wafanyakazi wa Benki ya NMB Tawi la Singida ikiwa ni mwendelezo wa Wiki ya Huduma kwa Wateja.

Alisema kama benki itaweka mkakati wa kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi popote walipo, wataondokana na tabia ya kuhifadhi fedha majumbani ambako si salama.

Dendego alisema ni wakati wa mkoa huo kukua katika matumizi ya huduma za benki na kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan wa vijijini kwa kuongeza idadi ya mawakala na mashine za ATM.

"Mkipeleka huduma za kibenki maeneo ya vijijini yenye mzunguko mkubwa wa fedha, uzalishaji utaongezeka maradufu na usalama wa wananchi utaongezeka kwani wataepuka kuhifadhi fedha ndani na kutumia njia rahisi za kibenki katika utunzaji wa fedha zao," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Fatuma Mganga, alisema ni wakati wa wananchi kunufaika na huduma za benki hasa wa vijijini wanaojishughulisha na uzalishaji mali kwa kufunguliwa akaunti na kupewa elimu juu ya matumizi ya huduma hizo.

Alisema elimu ya huduma hizo zinatolewa pia katika vikundi mbalimbali ili kuwapa utayari wa kuthubutu kutumia huduma za benki zenye gharama nafuu na usalama wa kutosha.

Meneja wa benki hiyo mkoani Singida, Emmanuel Kushosha, aliahidi kutoa ushirikiano kuhakikisha wanayafikia maeneo yote kwa kuweka tawi la benki.

"Tutahakikisha wananchi wanafikiwa na huduma za kifedha mahali popote na wakati wowote kwa kuongeza idadi ya mawakala wakubwa mjini na vijijini pia uwepo wa ATM zitakazorahisisha upatikanaji wa fedha kwa urahisi na usalama zaidi," alisema.



# Tanzania mbioni kuzalisha umeme wa jotoardhi

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imeanza kuhakiki jotoardhi katika maeneo ya mikoa ya Mbeya na Songwe kabla ya kuanza kuchoronga visima vya kuzalisha umeme kutokana na rasilimali hiyo.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Shakiru Idrisa Kajugusi, aliyasema hayo jana mbele ya wajumbe wa Kongamano la 10 la Jotoardhi Afrika lililofanyika jijini Dar es Salaam na kutembelea maeneo hayo matatu yenye rasilimali hiyo katika mikoa hiyo.

Kajugusi, aliyataja maeneo hayo kuwa ni Kyejo/Mbaka na Ziwa Ngosi ya Mbeya na Majimoto Kijiji cha Nanyara cha Songwe.

Alisema utafiti umebaini eneo la Ziwa Ngosi kuna rasilimali yenye uwezo wa kuzalisha umeme megawati 70, Kyejo/Mbaka 60 na Majimoto kati ya tano na 38.

"Utafiti huu tumeufanya tukiwa juu ya ardhi kwa kutumia vifaa mbalimbali vya kitafiti ikiwamo kupiga picha za kijiolojia na umeonekana rasilimali ipo ya kutosha, sasa tumeanza kuchoronga miamba kwa lengo la kuhakiki uwepo wa rasilimali hiyo na baada ya hapo tutaingia katika hatua ya mwisho ya kuanza uzalishaji wa umeme," alisema.

Alisema ikiwa hatua ya uhakiki wa rasilimali hiyo itamalizika kwa mafanikio, inayofuata ya kuchoronga visima vya kuzalisha umeme.

Alisema wanatarajia ifikapo mwaka 2028, wataanza kuzalisha megawati ya kwanza itokanayo na umeme wa jotoardhi nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TGDC, Mhandisi Mathew Mwangomba, alisema katika hatua hiyo ya uhakiki, watachoronga kisima chenye urefu wa mita 25,000 eneo la ziwa hilo.

Mwangomba, alisema wakifikia umbali huo chini ya ardhi, wanatarajia kupata joto la sentigredi 200 ambalo litawahakikishia uwepo wa rasilimali ya kutosha kuzalisha umeme wa jotoardhi.

Meneja Mradi wa Jotoardhi wa Ziwa Ngosi, Mhandisi John Lubuva, alisema mradi huo utakuwa na manufaa mengine kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo.

Alisema kutakuwapo na miradi mingine midogo midogo ambayo itawaingizia wananchi kipato.

Alizitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni ufugaji samaki, kilimo cha mboga, matunda na ya kukausha mazao kwa kutumia mvuke.

Wataalamu na wawekezaji kutoka mataifa zaidi ya 20 duniani waliohudhuria Kongamano la 10 la Jotoardhi Afrika lenye lengo la kuongeza kasi ya uendelezaji rasilimali hiyo Afrika wametembelea miradi miwili ya uendelezaji jotoardhi ya Kyejo/Mbaka na Ziwa Ngosi kujionea hatua ambayo Tanzania imefikia.



Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu (wa tatu kulia) na viongozi wenzake wakiangalia eneo la Mto Mnenje, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma juzi, ambalo linahitaji kujengwa daraja na kuahidi kushirikiana na wananchi katika ujenzi wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanakijiji waaga adha ya maji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Kijiji cha Soweto kilichoko Kata ya Kasanga wilayani hapa Mkoa wa Mbeya wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kuteka maji baada ya serikali kujenga mradi wa kisima.

Mradi huo umetekelezwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kwa kushirikiana na Shirika lisilokuwa la kiserikali la CRS kwa lengo la kutatua kero hiyo katika kijiji hicho.

Wakizungumza na Nipashe juzi baadhi ya wakazi hao, walisema kabla ya mradi huo kukamilika, walikuwa wanahangaika kutafuta maji hasa kipindi cha kiangazi kutokana na ukame.

Mmoja wa wakazi hao, Neema Sione, alisema walikuwa wanalazimika kutumia maji ya kwenye makorongo kwa kuchangia na wanyama, hivyo kuhatarisha afya zao.

Neema, alisema baada ya mradi huo kukamilika wameanza kupata maji jirani na makazi yao hali na kupunguza ugomvi wa familia na waume zao.

"Tunaishukuru serikali kwa mradi huu maana sasa tunaona uhalisia wa kauli ya kumtua mama ndoo kichwani, hapa tunachota maji kwenye maeneo ya jirani sana na nyumba zetu," alisema Neema.

Kaimu Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Chunya, Olineno Sanga, alisema kukamilika kwa miradi ya visima kumeongeza kiwango cha upatikanaji maji kutoka asilimia 32 mpaka asilimia 52.

Sanga, alisema wanaendelea na utekelezaji wa miradi katika maeneo mengine ili kuhakikisha wanatatua tatizo la upungufu wa maji kwa Chunya.

# Wahimizwa kutumia vituo vya afya vya serikali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI mkoani hapa wametakiwa kujenga mazoea ya kutumia vituo vya afya vya serikali kupata huduma baada ya kuboreshwa na kuwa na vifaa tiba vya kisasa na dawa.

Wito huo ulitolewa juzi na Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omary wakati akiwapokea madaktari bingwa na wabobezi 43 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakazi hao wa kwenye hospitali sita za halmashuari za mkoa huo.

Omary, alisema kuna tatizo la wananchi kujenga mazoe kwenda kupata huduma kwenye vituo vya afya binafsi badala ya hospitali za umma kutokana na dhana potofu.

"Ujio wa madaktari hawa ni hamasa kubwa, njooni mtumie huduma za vituo vya afya vya serikali ambavyo vimejengwa, vingine ni vipya na vifaa vimepokelewa vingi vinahitaji kutumika," alisema.

Omary, aliwataka wakazi hao kutumia fursa ya madaktari hao kwenda kupima, kuchunguzwa afya na kupata tiba kwa sababu kuna nyenzo za kutosha.

Daktari bingwa wa masuala ya uzazi pingamizi na masuala yote yanayohusiana na changamoto za uzazi, Nicolaus Kapunga, alisema serikali imefanya jitihada kuongeza vituo vya afya, vifaa tiba na utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Ujio wa madaktari bingwa iwe ni njia itakayowasaidia wananchi wengi kupata huduma ambazo walizikosa, madaktari tutasambaa kwenye hospitali mbalimbali za halmashauri na muunganiko huu unamsaidia mwananchi kujua anapaswa kumuona daktari yupi kwa ajili ya tatizo lake," alisema Kapunga.

Ofisa wa Programu ya Mama na Mtoto Wizara ya Afya, Cephlen Budodi, alisema kampeni hiyo inafanyika kwa awamu ya pili kwa mikoa yote ya Tanzania Bara na halmashauri 184.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. Juma Mfanga, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuleta madaktari hao kuwajengea uwezo watumishi kwenye hospitali hizo za umma baada ya kupelekewa vifaa tiba vya kisasa.

Madaktari hao wamepiga kambi kwa siku sita mkoani hapa kuanzia Jumatatu ya wiki hii hadi Jumamosi.





# CCM kumrudisha kundini Shamte

**Na Rahma Suleiman, Zanzibar**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema taratibu za kumrudishia uanachama mwanasiasa mkongwe, Baraka Mohamed Shamte zitaelekezwa kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho.

Vilevile chama hicho, kimesema uamuzi wa Baraka ambaye ni mtoto wa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Zanzibar (Uhuru Bandia) wa kuzungumzia maendeleo yanayoonekana visiwani hapa, ameonyesha uungwana baada ya kufahamu ukweli.

Hayo yalisemwa na Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi ya chama hicho, Khamis Mbetto Khamis katika taarifa yake kwa vyombo vya habari visiwani hapa juzi.

Mbetto, alisema maneno aliyotamka Baraka kuhusu maendeleo ya Zanzibar, hana wasiwasi wa kurudishiwa uanachama wake.

Alisema mwanasiasa huyo amekitumikia Chama cha Afro Shirazi (ASP) na baadaye CCM, aliteleza wakati fulani kama binadamu na sasa amejisahihisha, hivyo atarudi katika chama chake cha asili cha Mapinduzi.

"Ametambua juhudi na malengo ya Serikali ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi. Taratibu za kumrudishia rasmi uanachama wake zitaelekezwa na kupokewa kwa heshima zote," alisema Mbetto.

Alimtaja mwanasiasa huyo kuwa ni mdau muhimu wa maendeleo, hivyo kutokana na kutambua ufanisi wa kazi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), amechomoza na kuonyesha hisia zake za kizalendo.

"Amekuwa naibu katibu mkuu ASP Youth League. Akawa katibu wa CCM wilaya. Mwenezi wilaya ya Mjini. Alipovuliwa uanachama hakuyumba, akawa muungwana, hivyo taratibu zitaelekezwa kumrudishia uanachama wake," alisisitiza Mbetto.

Alisema mwanasiasa huyo kila wakati amekuwa mtetezi wa sera za CCM, hata alipofuatwa na vyama vya siasa kumwomba ajiunge navyo, alikataa.

"Ameridhia na utendaji wa Serikali ya Dk. Mwinyi inavyochapakazi, amekubali ukweli kutokana na dhamira ya kujenga nchi na kutumikia wananchi wa Zanzibar," alisema.

Mbetto, alisema CCM kwa kutambua historia ya Mzee Shamte na mchango wake kwa Zanzibar, maelekezo ya vikao vya kikatiba vitafanyika ili kukidhi matakwa na kutoa uamuzi mwingine.

"Awali hakutambua malengo na nia ya Rais Dk. Mwinyi haraka... kujikwaa si kuanguka, ameelewa, amejisahihisha na sasa atashirikishwa ili kusukuma mbele gurudumu la maendeleo," alisema.

## Serikali yajizatiti kidigitali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI imeimarisha mifumo ya kidigitali kuendana na kasi ya maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayoendelea duniani ili kurahisisha utendaji katika taasisi zake.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora nchini, Juma Mkomi, wakati akifungua mafunzo kwa maofisa wa serikali 450 wa TEHAMA nchini visiwani hapa

Mkoni, alisema mafunzo hayo yanalenga kuongeza ujuzi wa watumishi wa kada ya teknolojia hiyo serikalini kwa lengo la kuwaongezea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema mafunzo hayo pia yanatawajengea uwezo viongozi wa serikali kwenye teknolojia ya habari na kufanya maamuzi sahihi ya miongozo ya kisera na kufikiwa mkakati wa mwaka 2024 hadi 2034 kuchangia maendeleo ya uchumi wa kidigitali nchini.

Katibu mkuu huyo, alisema Tume ya TEHAMA ilifanya tathmini mwaka 2020 na kubaini ukuaji uchumi sekta za utoaji huduma na uzalishaji na hitaji la ongezeko la ujuzi wa teknolojia za kidigitali zinazoibukia.

Alisema tathmini hizo zimeweza kuipa serikali maono na kubaini maeneo ya kitaaluma ya TEHAMA zinazohitaji kujengewa uwezo na kuimarishwa kwa kuwa na wataalamu wa kutosha.

"Matokeo ya jitihada hizi ni kuwapo kwa mikakati ya utekelezaji wa mafunzo kwa ajili ya maendeleo ya TEHAMA nchini. Nafurahi kutambua utekelezaji wa mafunzo haya unafanyika ndani ya nchi kwa kutumia vituo vya mafunzo vilivyoko Dar es Saalam, Zanzibar, Mwanza na Arusha," alisema Mkomi na kusisitiza kuwa: "Hii inaonesha azma ya serikali kuwajengea uwezo watendaji wake badala ya kuwapeleka nje ya nchi kupata mafunzo haya."



Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shedrack Mziray (kulia) na Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani, Omari Mwanga, wakiangalia moja ya redio zinazotumia mionzi ya jua, zitakazotumika kusikiliza vipindi vinavyotoa elimu ya kukabiliana na utapiamlo kwa kaya maskini, wakati wa uzinduzi wa mpango huo, wilayani humo, juzi. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# Wadau watakiwa kutangaza utalii kupitia historia ya Mjimkongwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka taasisi na wadau kutangaza historia ya Mjimkongwe ili kukuza sekta ya utalii na kuongeza mapato.

Othman aliyasema hayo ofisini kwake wakati akizungumza na Kamati ya Maandalizi ya Mashindano ya mbio za Marathon ya Kimataifa yanayotarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki hii.

Alisema mji huo una mambo mengi ya kihistoria ambayo hayatangazwi ipasavyo na kufahamika na wageni na wenyeji kutokana na kukosekana ubunifu wa wadau.

Aliitaka kamati hiyo na wadau wengine kuwa wabunifu kwa kuibua vivutio vya utalii katika mji huo kuingiza katika mashindano kama hayo ya kimataifa.

Othman, alisema kwa kufanya hivyo, watajenga uelewa kwa wenyeji na wageni na kuchangia kukuza biashara ya utalii katika eneo hilo.

Alitaja miongoni mwa mambo yanayohitaji kutangazwa kuwa ni historia ya majengo ya mji huo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano hayo, Hassan Mussa, alisema watautumia mji huo kama kivutio cha utalii kwa washiriki kupitia maeneo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Mussa, maeneo hayo ni Mtaa wa Darajani kuelekea Kiponda, Hamamni, Mkunazini, Barabara ya Soko Muhogo na kumalizia Forodhani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHERRIN ERNEST** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne nyenye index namba **S4771.0026** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **APEX SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2017. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIG/233298/2024.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**SALIMU MUSSA FAKI SAID** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE483365** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mnamo tarehe **08/06/2022.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/235136/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PLASIDI FRANCIS MASSAWE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **NS1513/0063** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SOMSOM SECONDARY** mwaka 2027. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Control No. 9910842631062.**

## KUPOTEA KWA CHETI




**TRYPHONE TITUS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index **No. S0546-0333** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **PAMBA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011, Cheti hiki kimepotea Jijini DODOMA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/38417/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VENANCE JOSHUA MWAMPOTE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1361/0174** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SAMORA MACHEL SECONDARY** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/235472/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NANCY JOSHUA SIBONIKE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4923/0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHEPHERD SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/235309/2024.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**KUDRA SALUM KILEMLA** anatangaza kupotelewa na Result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.0534-0533** iliyotolewa na **ST. ANTHONY'S MBAGALA SECONDARY** mwaka 2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/234591/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**SAMWEL ISHEMBE KWIYEYA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE 461168** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 14/03/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/SHI/10346/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRANK DEZIDELI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **P4771/0009** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **APEX SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021, Cheti hiki kimepotea Mkoani KAGERA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/48420/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HILLARY RUMISHAELI URASSA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T563CES aina ya SCANIA P94, Chassis **No. 04431812,** Engine **No. XXXXX0.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/48503/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NURDIN MOHAMED LACHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 839 CHU – TOYOTA COASTER.** Chassis namba **JT748BB427001052.** Engine namba **14B562598752.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/41026/2024.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 341 LA 2024**

**CITY MORTGAGE AND FINANCE CORPORATION LTD.............MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOAN PETEWR MWASANDUNDE..........MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**JOAN PETEWR MWASANDUBE – POPOTE ULIPO/MLIPO**

**CITY MORTGAGE AND FINANCE CORPORATION** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 05/11/2024 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya **Mh. J.W. SILLAS.** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hii leo tarehe 28 mwezi 10, 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26337 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JONAIS EDWARD SHAYO**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LAMECK FRED SHAO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21$^{st}$ day of NOVEMBER 2024.

**Dated at KOROGWE this 21st day of OCTOBER, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 23820 of 2024**

**In the matter of the estate of the late MASIMA DAUDI PAURO of Chinyika within Dodoma City**

**And**

**In the matter of Application for letters of administration by HILDA FELEGESI MBATA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 OF Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 31..........................day of 10...........................2024
Dated at Dodoma this 21 day of 10 ...............2024.

..................................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.26771 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**

**FRANCIS MATHIAS MKOKO————————DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**

**1. THOBIAS FRANCIS MKOKO———————PETITIONER**
**2..............................................**

**GENERAL CITATION**
**(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 04th day of NOVEMBER,2024.
Dated at Morogoro this 28TH day of OCTOBER 2024.

*PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE*
MOROGORO DISTRICT COURT

---

**THE UNITED REOUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGESTRATES' COURT OF ARUSHA ARUSHA**

**CIVIL CASE NO. 26606 OF 2024**

**HISSANIELY JOHN MGONJA ..................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**1$^{ST}$ HASSANIELY JOHN MGONJA ..........................DEFENDANT**
**2$^{ND}$ NMB BANK.**

**TO : HASSANIELY JOHN MGONJA OF ARUSHA**

**WHEREAS THE NAMED PLAINTIFF(S)** has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in the annexed, copy of the plaint.
**YOU ARE HEREBY NOTIFIED THAT** you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within 21 days of service of this notice upon you. (If there are more plaintiffs than one additional copies of your written statement of Defense must be filed sufficient for service on each of the defendants).
**TAKE NOTICE THAT,** thus case has been fixed for mention on the noon or thereafter 12th day of NOVEMBER 2024 at 08:30 O'clock in the for noon before
Hon E. Y. PHILLY Resident Magistrate.
**AND TAKE FURTHER NOTICE THAT,** if you default in filling your written statement of defense within the time specified the court may pronounce judgment against you.
Given under my Hand and Seal of the court, this 23 day of OCTOBER 2024

RESIDENT MAGISTRATE
ARUSHA

Copy to:...................................................................

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA**

**MAOMBI NA. 53/2024**

**TUNTUFYE ASUKENYE MWANDUNGA (Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu ASUKENYE JAMES MWANDUNGA..................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **WILSON JOHN LEMWAI (Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu JOHN YONA LEMWAI...MJIBU MAOMBI**
2. **WILLIAM MASU................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA WILLIAM MASU**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kilosa tarehe 21/11/2024 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hutahudhuria, maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.
Imesainiwa leo tarehe 16 mwezi 10 Mwaka 2024.

SALEHE M. SHENGOTTO
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
KILOSA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 27046 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late ISSAKWISA GIDEON MWASANJOBE**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY HOBOKELA ANYIMIKE MWASAMWENE**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 11, 2024
Dated at Dodoma this 21 Day of October, 2024.

PETITIONER
**Presented for filling this 29 Day of 10, 2024**

RESIDENT MAGISTRATE

---


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARIKIMATAIFA

# Kamala Harris awakumbusha Wamarekani mabaya ya Trump

**WASHINGTON, Marekani**

WAGOMBEA wa urais wa Marekani, wanaongeza kasi ya kampeni zao, mgombea wa Chama cha Democtat, Kamala Harris, ametumia hotuba yake kuu ya mwisho kwa kuwakumbusha wapiga kura kuhusu maisha ya mgawanyiko wakati wa uongozi wa Donald Trump.

Aliwataka Wamarekani kuchagua kuishi katika maisha hayo, au kusonga mbele katika njia sahihi kama watamchagua yeye kuongoza taifa hilo lenye nguvu kubwa duniani.

Akizungumza mbele ya umati wa watu katika bustani iliyoko karibu na Ikulu ya White House na Mnara wa Washington, Harris alisema atawasikiliza Wamarekani wakati wote hata kama hawatompigia kura.

Alichagua eneo hilo lililoko mjini Washington DC, kwa sababu ndilo ambalo Trump alitumia kuwahutubia wafuasi wake kuwachochea kuvamia jengo la Bunge mnamo Januari 6, 2021.

Alisema Trump ametumia muongo mmoja uliopita kujaribu kuwagawanya wamarekani na anataka kurejea Ikulu ya White House sio kuangalia matatizo yao bali matatizo yake.

Harris aliwaambia mpinzani wake huyo anatafuta madaraka yasiyodhibitiwa, jambo ambalo ni hatari.

„Tunamfahamu Donald Trump ni nani, alilituma kundi la watu wenye silaha kulivamia bunge la Marekani katika jaribio la kuyabatilisha matokeo ya uchaguzi wa 2020, alisema.

Mkuu wa Ofisi ya DW mjini Washington, Ines Pohl, alisema hotuba hiyo huenda ikazingatiwa kama moja ya hotuba zenye nguvu zaidi alizowahi kutoa mpaka sasa.

Alisema Harris alijipambanua kama mtetezi mwenye nguvu wa haki za wanawake, ambaye alifanikiwa maishani kupitia bidii bila msaada wa mali.

Hotuba hiyo iliyoelezwa kuhudhuriwa na watu zaidi ya 70,000 ilielezwa kwamba itatosha kuwashawishi wapigaji kura ambao hawajaamua katika uchaguzi utakaofanyika wiki inajayo.

Hata hivyo, mgombea wa Republican, Donald Trump, alijibu hutuba hiyo kwa kusema mpinzani wake Kamala Harris, anang'ang'ania matukio yaliyopita.

Timu ya Kampeni za Trump, ilisema hotuba ya Harris ilikuwa ya kuirudisha nchi nyuma.

Msemaji wa kampeni za Trump, Karoline Leavitt alisema Harris anadanganya, anachafua majina ya watu na kung'ang'ania yaliyopita ili kukwepa ukweli kwamba mgogoro wa wahamiaji, mfumuko wa bei na vita vinavyotokota ulimwenguni vinatokana na sera zake mbovu.

Pia alibaini kuwa Harris amekuwa ofisini kwa karibu miaka minne, lakini hakuna kinachoonekana cha mafanikio.

***DW***



Mfalme wa Morocco, Mohammed VI (kulia) na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, wakisalimia watu waliojipanga barabarani katika jiji la Rabat wakati wa ziara rasmi ya rais huyo, Morocco iliyoanza juzi. **PICHA: AP**

# Marekani yashtushwa mauaji watu 93 Gaza

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imelitaja shambulio lililofanywa na jeshi la Israel katika Ukanda wa Gaza na kuu watu 93, kuua ni vibaya na kuogopesha. Mashambulizi hayo ya anga yalilenga jengo moja la ghorofa tano katika mji wa Beit Lahia kaskazini mwa Gaza.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Matthew Miller, alisema Marekani imesikitishwa na tukio hilo ambalo limepoteza maisha ya raia wengi.

"Hili lilikuwa tukio la kuogopesha na matokeo ya kuogofya". Alisema.

Waokoaji walisema jengo hilo liliangushwa chini huku maiti zikiwa zimetapakaa na zingine kufukikwa kwenye kifusu.

Video kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha miili ya watu iliyofunikwa kwa blanketi ikiwa imelazwa sakafuni.

Jeshi la Israel lilisema linafahamu ripoti kwamba raia walijeruhiwa katika eneo la Beit Lahia na kuongeza kuwa taarifa za tukio hilo zinapitiwa upya.

Vikosi vya Ulinzi vya Israel (IDF) vimekuwa vikifanya kazi kaskazini mwa Gaza katika muda wa wiki mbili zilizopita, hasa katika maeneo ya Jabalia, Beit Lahia na Beit Hanoun.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Kamal Adwan iliyoko Jabalia, Hussam Abu Safia, ameliambia shirika la habari la AFP kwamba watoto walikuwa wakitibiwa katika hospitali hiyo ambayo inashindwa kuwatibu wagonjwa kutokana na ukosefu wa wafanyakazi na dawa.

„Hakuna kilichosalia katika Hospitali ya Kamal Adwan isipokuwa vifaa vya huduma ya kwanza baada ya jeshi kukamata timu yetu ya matibabu na wafanyakazi," alisema Abu Safia. IDF ilivamia hospitali hiyo wiki iliyopita, ikisema ilikuwa ikitumiwa na wapiganaji wa Hamas.

Israel ilisema operesheni zake kaskazini mwa Gaza zimefanyika ili kuzuia Hamas kujipanga upya na inawatuhumu kwa kujiingiza ndani ya jimii, jambo ambalo Hamas inakanusha.

***BBC***

## Ufaransa, Morocco wafungua sura mpya kuchochea uchumi

**RABAT, Morocco**

MFALME Mohammed VI wa Morroco na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, wamefungua sura mpya katika historia ya mataifa hayo kwa kuboresha uhusiano ili kukabiliana na changamoto za pamoja za kikanda na kimataifa.

Makubaliano hayo yamefikiwa wakati wa ziara ya Macron nchini Morocco iliyofanyika wiki hii, ambayo ililenga kuanzisha uhusiano imara na wa kipekee.

Wakati wa ziara hiyo, Macron alisisitiza uungaji mkono wa Ufaransa kwa Morocco juu ya suala la Sahara Magharibi, akisisitiza umuhimu wa heshima ya pande zote na ushirikiano katika uhusiano wao.

Viongozi hao walisaini makubaliano mapya 22 yanayolenga kuimarisha ushirikiano katika sekta mbalimbali.

Makubaliano mapya yaliyofikiwa yanadhihirisha azma ya pamoja ya kuimarisha uhusiano wa kihistoria na kitamaduni kati ya mataifa hayo mawili.

Ushirikiano huo unalenga kukabiliana na changamoto za kimkakati na kukuza maendeleo ya kiuchumi, umoja wa kijamii na maadili ya pamoja.

Maeneo muhimu wa ushirikiano ni pamoja na mwelekeo wa kisiasa na kimkakati ili kukabiliana kwa ufanisi na changamoto kubwa za kimataifa, kuboresha na kuendeleza uchumi, hasa katika usalama wa afya, kilimo, miundombinu na nishati mbadala.

Viongozi hao pia walikiri umuhimu wa kuimarisha ushirikiano katika usimamizi wa uhamiaji, wakitetea uhamaji wa kisheria wakati wa kupambana na uhamiaji usio wa kisheria.

Kikatiba, walisisitiza umuhimu wa Afrika, uhusiano wa Euro-Mediterranea, na Mashariki ya Kati katika mazungumzo yao ya kimkakati.

Pia viongozi hao walikubaliana kukuza mipango ya pamoja inayolenga kuimarisha utulivu na maendeleo katika maeneo haya.

Katika uwanja wa kimataifa, Macron na Mohammed VI walionyesha kujitolea kwao kutatua migogoro ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na changamoto za mazingira na kutafuta suluhu za migogoro, wakiangazia hasa Afrika.

Katika kuthibitisha msaada wa Ufaransa, Macron alisisitiza kwamba mustakabali wa Sahara Magharibi uko ndani ya mfumo wa uaminifu wa Morocco.

Alisema kuwa uhuru chini ya utawala wa Morocco ni njia ya kupata suluhu ya haki na ya kudumu.

***AFP***

HABARI MICHEZO

# KMKM, New City FC vitani Ligi Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM SC inatarajia kukutana na New City katika mechi ya raundi ya tisa ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex ulioko visiwani hapa.

KMKM inashuka dimbani huku ikihitaji kuendelea kujiimarisha katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar wakati wapinzani wao New City wanataka pointi tatu muhimu zitakazowasaidia kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema mchezo huo anajua hautakuwa rahisi kama mashabiki na wadau wanavyoufikiria.

Msimu alisema wanaenda kucheza na timu ambayo iko chini katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, hivyo watakuja na mbinu kali ya ushambuliaji ili kupata matokeo chanya.

Kocha huyo alisema amekiandaa kikosi chake kucheza soka la utulivu na kuepuka kuingia mtegoni kwa wapinzani wao ambao wanazihitaji zaidi pointi tatu za mechi hiyo.

"Tunafahamu mechi zote ni ngumu, lakini hii mchezo huu haitakuwa rahisi zaidi kwa sababu tunatarajia kuona wapinzani wakitupa ushindani, sisi tumejiandaa kuwakabili kwa mbinu yoyote ambayo wataingia nayo," alisema Msimu.

Aliongeza wachezaji wake wote wa kikosi cha kwanza wako tayari kwa mchezo huo na hana mchezaji ambaye ni majeruhi.

"Nimewafuatilia wapinzani wangu katika michezo yao kadhaa ya Ligi Kuu, nimebaini wana wachezaji wazuri hivyo hatutabweteka katika mchezo huo. Mara nyingi unapocheza na timu ambayo imeanza vibaya katika michezo iliyopita, mchezo unaofuata unatarajiwa kuwa mgumu kwa sababu wanataka kuhakikisha wanapata alama tatu za kuwatoa sehemu waliyopo, hivyo tumejiandaa kukabiliana nalo," Msimu alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM ipo kwenye nafasi ya tatu ikiwa na alama 15 kibindoni wakati New City FC wenye pointi tano wapo nafasi ya 14 kati ya timu 16 zinazoshiriki ligi hiyo.

# SABABU YANGA, AZAM FC KURUDISHWA DAR YATAJWA

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, amesema mechi ya Yanga dhidi ya Azam FC iliyotarajiwa kuchezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa New Amaan Zanzibar sasa itachezwa Azam Complex, Dar es Salaam kutokana na matakwa ya kanuni.

Kanuni zinaelekea mwenyeji anatakiwa kuchagua uwanja wa pili wa nyumbani ndani ya siku 21.

Akizungumza jijini jana, Kasongo alisema kufuatia mchezo namba 87 kati ya timu hizo mbili kupelekwa uwanja huo ulioko Chamazi, badala ya Uwanja wa Benjamin Mkapa uliopangiwa awali.

Kasongo alisema Yanga ambayo kikanuni inatumia Uwanja wa Benjamin Mkapa na Azam Complex kama viwanja vyake vya nyumbani, ili mechi ikubaliwe kwenda New Amaan Complex, Zanzibar kikanuni maombi yao yalipaswa yawe ya angalau siku 21 kabla.

"Kikanuni Yanga itaendelea kucheza kwenye viwanja ambavyo inavitumia kwa mechi za nyumbani, na ukiondoa Benjamin Mkapa, unaofuata ni Azam Complex, kwa hiyo Bodi ya Ligi kwa kushirikiana na Yanga na mmiliki wa uwanja, kwa sasa tuko katika hatua za mwisho kuangalia mechi hiyo tunaichezaje hapo.

Hii ni pamoja na kuzingatia idadi ya mashabiki, viingilio, kwa sababu wamiliki wameshafunga viti, kwa maana hiyo hata ule uwezo wa kuingiza watu wengi zaidi kama zamani umepungua kidogo," Kasongo alisema.

Alitaja pia sababu za kuutoa Uwanja wa Benjamin Mkapa ni kutokana na kuwapo kwa matengenezo, hivyo maombi ya wenyeji wa mchezo huo hayakukubaliwa.

„Wenyeji wa mchezo waliomba mchezo huo uchezwe kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, maombi yao hayakukubaliwa, lakini unaweza kuelewa uwanja upo katika matengenezo makubwa, wakandarasi wanahitaji muda zaidi, imeonekana itakuwa changamoto kumsimamisha kwa ajili ya mchezo huo," Kasongo alisema.

Wakati kikanuni Yanga ikiwa mwenyeji wa mchezo huo, uwanja huo unamikiliwa na Azam FC, hivyo kila timu itajihisi kama ipo nyumbani.

Pamoja na hayo, Yanga ina rekodi nzuri zaidi kushinda mechi zake dhidi ya Azam inapocheza kwenye uwanja huo, huku Wanalambalamba wenyewe wakiwa na rekodi nzuri na Wanajangwani hao wanapocheza Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na jana usiku walitarajiwa kukutana na Singida Black Stars katika mechi ya ligi hiyo iliyopangwa kufanyika kwenye Uwanja wa New Amaan Complex.



Wachezaji wa Dodoma Jiji wakishangilia baada ya timu yao kufunga bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KenGold iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya mapema wiki hii. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# Kipanga FC yajipa matumaini

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WANAJESHI wa Kipanga FC wamesema bado wana nafasi ya kufanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar licha ya sasa kupata matokeo mabaya katika ligi hiyo yenye timu 16.

Kipanga yenye pointi saba iko katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kushinda mechi mbili, kutoka sare mchezo mmoja na imefungwa michezo minne.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Kipanga FC, Jaffar Idd, alisema kwa sasa wanajipanga kuhakikisha wanafanya vyema na kurejesha furaha kwa mashabiki wao.

Idd alisema wanaendelea kufanyia kazi makosa waliyoyabaini na kuhakikisha wanajiweka kwenye nafasi nzuri kabla ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

"Mipango yetu ni kuhakikisha michezo yetu nane iliyobakia tunashinda ili kupata alama ya kutusogeza juu katika msimamo wa ligi, tunaamini hili linawezekana," alisema Idd.

Aliongeza anajua ugumu wa ligi hiyo hasa katika mzunguko wa awali na wanaendelea kujiimarisha ili kufikia malengo.

"Vita kuu iliyoko ni ya kuwania ubingwa ingawa timu yetu bado ni mapema kusema kama hatupo au tumo katika mbio hizo kutokana na nafasi tuliyopo na matokeo ya michezo iliyopita," Idd alisema.

Kipanga itashuka tena dimbani kuwakabili Inter Zanzibar FC katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBEUMO ATAJWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Brentford na Timu ya Taifa ya Cameroon, Bryan Mbeumo, mwenye umri wa miaka 25, ifikapo Januari lakini Magpies wanakabiliwa na vikwazo vya matumizi ya fedha. ***(Telegraph)***

### AMORIM ANUKIA UNITED
KLABU ya Manchester United inatarajia kumteua Kocha wa Sporting, Ruben Amorim, kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Old Trafford. ***(Mail)***

### CITY YAMTAKA GUARDIOLA
MABOSI wa Manchester City wamesema bado inaweka matumaini kwa Pep Guardiola ataongeza muda wake kama kocha na klabu hiyo. ***(Mail,}***

### UNITED KUSAJILI JANUARI
YEYOTE atakayemrithi Erik ten Hag kama Kocha wa Manchester United atakuwa na bajeti ndogo ya kuimarisha kikosi katika dirisha dogo la usajili litakalofunguliwa Januari. ***(Guardian)***

### DAVIES AKARIBIA MADRID
KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumsajili beki wa pembeni wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 23, Alphonso Davies, lakini mchezaji huyo yuko mbioni kuhamia Real Madrid. ***(Sky Sports Switzerland, Via Give Me Sport)***

### ARSENAL YAMFUATA SANE
KLABU ya Arsenal inashughulikia mpango wa kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane, mwenye umri wa miaka 28, wakati mkataba wake wa Bayern Munich utakapokamilika msimu ujao. ***(Football Insider)***,

### SPORTING KUMUUZA GYOKERES
KLABU ya Sporting iko tayari kumuuza, Viktor Gyokeres, kwa dau la kati ya pauni milioni 50 na 58 ifikapo msimu ujao, huku Manchester City, Arsenal, Liverpool na Chelsea zikimhitaji mshambuliaji huyo wa Sweden mwenye umri wa miaka 26***. (Florian Plettenberg)***,

### UNITED KUMUUZA ANTONY
KLABU ya Manchester United itapunguza hasara yao kwa winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, kwa pauni milioni 86 baada ya Erik ten Hag kutimuliwa. ***(Sportsport)***

### WERNER NJIA MOJA
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, anaegemea kumtoa fowadi Mjerumani Timo Werner, mwenye umri wa miaka 28, ifikapo mwishoni wa msimu. ***(GiveMeSport)***

### WEST MAMBO MAGUMU
KLABU ya West Ham haina uwezekano wa kuwa na fedha za kutumia katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# AMORIM AFUNGUKA KUTUA OLD TRAFFORD

●●● Lakini kocha huyo Mtaliano akiri bado hawajafikia mwafaka...

**LISBON, Ureno**

KOCHA wa Sporting CP, Rúben Amorim, amekiri nia ya Manchester United ya kumfanya kuwa kocha mpya wa klabu hiyo ya Ligi Kuu England lakini akasisitiza bado hajaamua kuhamia Old Trafford.

Mkataba huo ulikaribia mapema juzi huku klabu hiyo ya Ureno ikifahamisha mdhibiti wa fedha wa nchi hiyo United walikuwa wamethibitisha nia yao ya kulipa pauni milioni 10 ya kifungu cha kutolewa cha Amorim.

Vyanzo vimeiambia ESPN, United wamedhamiria kumpa mkataba kocha huyo mwenye sifa ya juu zaidi kuchukua nafasi ya Erik ten Hag kabla ya mechi ya Jumapili dhidi ya Chelsea.

Akizungumza baada ya ushindi wa mabao 3-1 wa timu yake dhidi ya Nacional kwenye Taca da Liga juzi usiku, Amorim alisema hatakuwa sehemu ya mchezo wa Sporting Primeira Liga dhidi ya Estreia Armadora utakaochezwa kesho kama atafikia mwafaka.

"Kulikuwa na taarifa ya klabu na ndicho kitu pekee kilichoko kwa sasa," alisema.

"Kuna nia kutoka kwa Manchester United. Lakini lazima liwe chaguo langu. Mpaka kila kitu kitakapoamuliwa, hatutaleta kelele. Sina la kusema. Nitachukua chochote ninachotaka kufanya, kama ninavyofanya siku zote.

"Kuna klabu imeonesha nia na imewasiliana na klabu tangu na iko tayari kulipa kifungu cha kutolewa. Hilo siwezi kulidhibiti, tutaona kitakachotokea siku chache zijazo, lengo langu kesho (leo), ni kujiandaa kwa mchezo wa Ijumaa dhidi ya Estreia Armadora.


"Hakuna asiyejua kama ni mchezo wa kuaga, kutakuwa na mchezo wa kuaga ni kitu ambacho bado hakijaamuliwa, tuchambue mchezo, nikishafanya maamuzi nitatoka na kueleza uamuzi wangu.

"Kama taarifa ya klabu ilisema, itakuwa uamuzi wangu. Lakini kusema mambo nusu sasa haionekani kuwa bora."

HABARI MICHEZO

# Arne Slot: Chiesa hatolewi mkopo

**LIVERPOOL, England**



KOCHA wa Liverpool, Arne Slot, amekiri masuala ya utimamu wa mwili yanaendelea kumsumbua mchezaji aliyesajiliwa majira ya kiangazi, Federico Chiesa, lakini akakanusha uvumi winga huyo huenda akatolewa kwa mkopo ifikapo Januari.

Chiesa alikamilisha uhamisho wa pauni milioni 10 kutua hapo Anfield msimu wa joto akitokea Juve, lakini amecheza kwa dakika 78 tu katika mechi tatu hadi sasa msimu huu na hajajumuishwa katika kikosi cha siku ya mechi kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Ripoti zilidokeza Liverpool inaweza kumrudisha Chiesa kwa mkopo Italia katika dirisha la uhamisho la Januari na Slot amepuuzia mbali uvumi huo, alikiri Chiesa yuko kwenye vita vya kweli vya kujiweka sawa.

"Kuachana na Chiesa haijapita akilini mwangu hata kidogo," alisema Slot.

"Kwanza kabisa anapamba kuwa fiti tena ndipo tuone alipo.

"Alikosa mechi za kujiandaa na msimu mpya akiwa na Liverpool.

"Tulilijua hili hapo awali na tulijua tulipaswa kuwa waangalifu sana kuzoea mahitaji yake binafsi.

"Lakini bado haijawa kamilifu kwa hivyo tunajaribu kutafuta njia sahihi ya kumjenga bila kumzidishia mzigo.

Alipoulizwa ni lini Chiesa anaweza kurejea Liverpool, Slot alikiri: "Siku zote ni vigumu kusema anapopanda na kushuka. Wakati mwingine anakuwa nasi mazoezini kwa siku chache kisha anatoka nje kwa sababu ya jeraha tena.

"Sitaki kuweka siku au wiki juu yake kwa sababu lazima tuhakikishe anakuwa katika hali nzuri zaidi na tusimpe shinikizo kwa kuja na tarehe."

# Ronaldo atolewa Kombe la Mfalme



**RIYADH, Saudi Arabia**

AL Nassr imeondolewa katika michuano ya Kombe la Mfalme wa Saudia na Al Taawoun baada ya Cristiano Ronaldo kukosa penalti dakika za lala salama hapo juzi.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon D'Or bado hajashinda taji kubwa tangu ajiunge na klabu hiyo takriban miaka miwili iliyopita.

Al Taawoun ambao ni wageni katika Ligi Kuu ya Saudia walipata bao la kuongoza katika dakika ya 71 ya mechi ya raundi ya 16 iliyochezwa kwenye Uwanja wa A Al Awal Park mjini Riyadh kupitia kwa Waleed Al-Ahmed.


Huku mechi ikiielekea mwisho, Al Nassr walipata penalti mwishoni mwa dakika, lakini Ronaldo, ambaye hajawahi kukosa penalti kati ya 18 tangu ajiunge na SPL aligongesha mwamba.

Kipigo hicho ni cha kwanza kwa Kocha, Stefano Pioli, tangu Mtaliano huyo amrithi Luis Castro kama kocha mkuu tangu Septemba.

"Kiufundi tulifanya vyema lakini hatukushinda mchezo," alisema Piol.

"Tunajisikia kukata tamaa kuwa nje ya kombe hilo. Lakini bado tuna mataji mawili ya kutwaa na tutajitolea kwa uwezo wetu."

Nyota wa zamani wa Manchester United na Real Madrid, Ronaldo na Al Nassr bado wana nafasi mbili za kutwaa ubingwa msimu huu, lakini tayari wako pointi sita nyuma ya kiongozi Al-Hilal baada ya mechi nane za Ligi ya Saudia na wana pointi saba katika mechi tatu za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa ya Asia.



# MOURINHO: UEFA HAINITENDEI HAKI

**ANKARA, Uturuki**

JOSE Mourinho anaamini Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA) halimtendei haki sawa kama makocha wengine tangu fainali ya Ligi ya Europa ya mwaka jana.

Akiwa Kocha wa AS Roma, Mourinho mwaka jana alifungiwa mechi nne UEFA kwa kumtusi mwamuzi, Anthony Taylor, baada ya timu yake kushindwa kwa penalti dhidi ya Sevilla katika mechi ya Fainali ya Ligi ya Europa iliyochezwa mjini Budapest.

"Hisia ni kwamba, niko taabani Ulaya," alisema Mourinho akiliambia Sky Sports katika mahojiano yaliyofanyika juzi.

"Nilipoteza fainali kwa njia ambayo bado siikubali, na tangu wakati huo ninahisi.

"Sitaki kufanyiwa upendeleo maalum, nataka nitendewe kwa uaminifu. Ni hivyo tu. Kwa hiyo nikikosea niadhibu na nilipe, lakini nisipofanya kosa niachwe kwa amani, lakini inakuwa ngumu.

"Tangu fainali hiyo ya Budapest inazidi kuwa ngumu."

Mourinho, ambaye sasa anainoa Fenerbahce, alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja katika sare ya 1-1 na Manchester United wiki iliyopita kwenye mechi ya Ligi ya Europa.

Aliadhibiwa baada ya mzozo mkali na mwamuzi wakati upande wake ulikataliwa rufaa ya adhabu.

"Ninastahili kutendewa kama kila mtu mwingine," alisema Mourinho.

"Ukiwa uwanjani haijalishi wewe ni Lionel Messi au unacheza mechi yako ya kwanza. Kanuni ni sawa kwa Messi na mtoto mdogo. Na kwa makocha ni kitu kimoja.

"Haijalishi kama wewe ni Carlo Ancelotti au kocha mchanga ndio unaanza. Ancelotti lazima awe na tabia sawa na kocha mwingine.

"Hicho ndicho ninachotaka mimi mwenyewe, na ndicho ambacho sipati."

Mourinho alisema baada ya mechi dhidi ya United kazi yake inayofuata atalazimika kuwa katika klabu ya England ambayo haishiriki mashindano ya UEFA.

HABARI MICHEZO

# RAIS MWINYI MGENI RASMI MBIO ZA TIGO-ZANTEL 2024

**Na Faustine Feliciane**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Tigo-Zantel Zanzibar Marathon 2024 zilizopangwa kufanyika keshokutwa visiwani humo.

Huu ni msimu wa nne mfululizo wa mbio hizo zinazotarajiwa kushirikisha wanariadha kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania ambao watashindana kuanzia umbali wa kilomita tano, kilomita 10 na kilometa 21 (nusu marathon).

Mkurugenzi wa Tigo- Zantel upande wa Zanzibar, Azizi Said Ali, alisema jijini jana kuwa maandalizi ya mbio hizo yanaendelea vizuri na tayari washiriki wameanza kujiandikisha kwenye vituo vilivyoko Dar es Salaam na Zanzibar. Ali alisema Rais Mwinyi amethibitisha atakuwa mgeni rasmi katika mbio za mwaka huu.

"Ni jambo la kujivunia kuona mkuu wa nchi anatambua faida ya watu kushiriki kwenye mazoezi na mashindano kama haya, siku ya mbio tunatarajia Rais Mwinyi kuwa mgeni rasmi," alisema Ali.

Alisema wanatarajia leo kuanza kupokea washiriki kutoka nje ya Zanzibar tayari kwa ajili ya kushiriki katika mbio hizo ambazo zitachochea uchumi wa wafanyabiashara na wajasiriamali.

"Muda wa kujiandikisha unaenda ukingoni, ambao bado wajitokeze, tunatarajia kuwa na idadi kubwa ya washiriki, wapo ambao wanatoka Kenya tayari wamethibitisha kushiriki na wamejiandikisha tayari," alisema mkurugenzi huyo.

Aliongeza ili kuzifanya mbio hizo kuwa katika kiwango cha juu, wamefanya maboresho mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha watu wajitokeze kwa wingi kushiriki.

"Tunawaomba watu wajitokeze kujiandikisha na kushiriki mbio hizi, muda bado upo, unaposhiriki unajiweka katika mazingira mazuri ya kuimarisha afya yako," aliongeza.



Golikipa wa KMC FC, Fabien Mutombora, akifanya mazoezi jana asubuhi kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha Namungo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Kapilima alia na mastraika

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA Mkuu wa KenGold FC, Omari Kapilima, amesema moja ya kazi ambayo anaenda kuifanya kwenye uwanja wa mazoezi ni kuinoa zaidi safu yake ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikipoteza nafasi wanazozitengeneza, imeelezwa.

Akizungumza baada ya mechi dhidi ya Dodoma Jiji FC ambayo ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2 hapo juzi, Kapilima, alisema timu yake ilicheza vizuri lakini waliangushwa na umakini mdogo wa washambuliaji.

"Nashukuru kwa kupata hata hii pointi moja, moja ya jambo ambalo nimeliona kwa upande wetu ni kutotumia vizuri nafasi nyingi tunazozitengeneza, tutarudi kwenye uwanja wa mazoezi kufanyia kazi kile ambacho nimekiona," alisema Kapilima, nyota wa zamani wa Yanga, Mtibwa na Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Maxime, alisema kabla ya mchezo huo alitambua angekutana na kibarua kigumu dhidi ya wapinzani wao.

Maxime alisema mchezo huo ulikuwa mgumu kutokana na mahitaji ya kila timu lakini anashukuru kwa kupata alama moja ya ugenini.

Matokeo hayo yameifanya KenGold FC kuendelea kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikifikisha pointi tano baada ya kucheza michezo 10 huku Dodoma Jiji ikibakia nafasi ya saba na pointi 13 kibindoni, ikicheza pia michezo 10.

## Simba SC yaitisha Mashujaa

INATOKA UK. 24

kupumzika wachezaji wangu, kiukweli walikuwa wamechoka kwa sababu ya kucheza mechi nyingi ndani ya muda mfupi, na wengine ni majeruhi," Fadlu alisema.

Aliongeza wachezaji wengine ambao si majeruhi wako tayari kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu.

"Najua hakuna mechi rahisi katika ligi, tuko tayari kupambana na kusaka matokeo mazuri, tunaamini tutafikia malengo yetu," alisema kocha huyo.

Wachezaji wa Simba ambao ni majeruhi na hawapo katika mpango wa mechi ya kesho ni Abdulrazack Hamza na Yusuph Kagoma, nyota hao waliumia katika mchezo wa watani wa jadi dhidi ya Yanga uliochezwa Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Gamondi ataka watatu wapya

INATOKA UK. 24

mara pamoja na Mzambia Kennedy Musonda huku upande wa beki ya kulia, amekuwa zaidi akimtumia, Yao Kwasi.

"Kuna wakati mwalimu amekuwa akimpa nafasi Shomari Kibwana, lakini ameona inafaa kuwaongezea nguvu katika maeneo hayo," alisema.

Mapema wiki hii straika, Kelvin Nashon alitajwa kukamilisha mazungumzo ya kujiunga na Yanga akitokea Singida Black Stars lakinio nyota huyo ameweka wazi bado hajafanya mazungumzo yoyote na mabingwa hao watetezi.

Yanga pia inahitaji kujiimarisha ili kufanya vyema katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Yanga imepangwa Kundi A pamoja na Al Hilal ya Sudan, TP Mazembe (Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo-DR Congo) na MC Alger ya Algeria.



Michezo
Alhamisi Oktoba 31, 2024
Nipashe

**Amorim afunguka kutua Old Trafford**
UKURASA 21



# SIMBA SC YAITISHA MASHUJAA

●●●Yatamba imewaandalia 'kipigo kikali' na kuwataka 'kutowazoea'...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeipiga mkwara mzito Mashujaa FC, ikisema ni timu ambayo inataka kuwazoea, hivyo imepanga kuwapa ‚kipigo kikali' katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana, wamejipanga imara kuhakikisha wanarudisha heshima yao.

Ahmed alisema Mashujaa FC wamekuwa na ‚dhihaka' kwao hasa baada ya msimu uliopita kuwatoa katika hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Kombe la Shirikisho na Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), maarufu Kombe la FA.

Katika mchezo huo, Maafande hao wa Mashujaa waliwaondoa Simba kwa penalti 6-5 baada ya timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida.

Meneja huyo alisema wameenda Kigoma ‚kuwafuta machozi' wanachama na mashabiki wao, ambao mara ya mwisho waliwaachia majonzi kutokana na matokeo ya kuumiza ya mchezo huo.

"Kikosi kitaondoka leo (jana), kwenda Kigoma, Mashujaa wanaonekana kutaka kutuzoea sasa, inampa kichwa kwa sababu walitutoa katika michuano ya Kombe la FA msimu uliopita, lakini wakumbuke Simba ile siyo hii ambayo ina maboresho makubwa, ni ya Fadlu Davis, Debora Fernandes Mavambo, Leonel Ateba, Moussa Camara, Jean Charles Ahoua na wengine.

Tunakwenda kuwafuta machozi wanachama mashabiki wa Simba Kigoma ambao mara ya mwisho tuliwaachia majonzi makubwa, safari hii tunakwenda kuchukua pointi tatu, hii ndiyo kampeni yetu kuanzia sasa," alisema Ahmed.

Hata hivyo, katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, rekodi zinaonyesha Simba imeshinda michezo yote miwili ya msimu iliopita.

Ilishinda bao 1 - 0 kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mechi iliyofanyika Februari 3, mwaka huu kabla ya kushinda mabao 2-0 katika mchezo wa mzunguko wa pili uliochezwa Machi 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Simba itashuka katika mchezo huo, baada ya kutocheza mechi dhidi ya JKT Tanzania ambao walipata ajali Jumapili iliyopita walipokuwa wakitoka Dodoma kuwakabili wenyeji Dodoma Jiji.

Baada ya Bodi ya Ligi (TPLB), kuahirisha mechi hiyo hadi itakapotangazwa siku nyingine, Simba iliendelea na mazoezi na jana asubuhi ilisafiri kwenda Kigoma ambapo iliwasili salama mkoani humo.

Naye Kocha Mkuu, Fadlu Davis, akisema kutokuwapo kwa mchezo huo kumesaidia kuwapa wachezaji wake mapumziko kwa sababu walikuwa na uchovu.

"Kutocheza mechi dhidi ya JKT Tanzania kwa upande wetu imetusaidia kuwapa nafasi ya

INAENDELEA UK. 23



Kiungo wa Simba, Deborah Mavambo

# Gamondi ataka wa3 wapya

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kikosi chake jana usiku kilishuka kucheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Black Stars kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameanza kupiga hesabu za kuongeza nguvu katika kikosi chake kwa kuhitaji kusajili wachezaji watatu wapya.

Taarifa kutoka ndani ya Yanga zinasema, Gamondi amepeleka maombi kwa uongozi wa klabu hiyo akipendekeza anataka kufanyika kwa mchakato wa kusajili nyota watatu wakati dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa ili kukiimarisha kikosi chake.

Chanzo chetu kilisema Gamondi amebaini kikosi chake kina mapungufu katika nafasi ya beki wa kulia, winga na mshambuliaji wa kati.

„Kocha Gamondi ameona kuna haja ya kukiongezea nguvu kikosi chetu, kuna mapendekezo amewapa viongozi ili wakati wa dirisha dogo wasajiliwe wachezaji watatu, na ameainisha maeneo ya kufanyiwa kazi, lengo anahitaji kupata mafanikio zaidi kwenye mashindano ya ndani na Ligi ya Mabingwa Afrika," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza kocha anatambua ushindani uliopo katika Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya kimataifa wanayoshiriki, hivyo lazima anahitaji kukiimarisha zaidi kikosi chake.

"Uongozi umeanza kufanyia kazi mapendekezo ya kocha, mambo yanafanywa chini kwa chini na ikifika dirisha dogo kila kitu kitakuwa wazi, wachezaji wanaofuatiliwa sasa watajulikana hapo baadaye muda rasmi ukifika," kiliongeza chanzo chetu.

Kilisema Gamondi anataka kuongeza nguvu katika eneo ushambuliaji ambalo kwa sasa straika, Clement Mzize, amekuwa akipata nafasi mara kwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >